

# KUMILIKI VITU VYOTE

 Kwa kweli ninashukuru sana kuwa hapa. Ninayathamini maombi yenu mliposikia ile ajali ndogo niliyopata. Inaonyesha tu ya kwamba Shetani hawezi kukuchukua mpaka Mungu amekuwa tayari. Na ninadhani wengi wenu mnashangaa jinsi ninii...kile kilichotukia. Daima nimependelewa...Kama mjuavyo mimi...burudani yangu, ama jinsi ninavyojiburudisha, ni ama kwenda kuvua samaki au kushuka kwenda mahali pa kupiga shabaha na kulenga risasi, ama kwenda kuwinda, ama kitu kama hicho. Ninafurahia jambo hilo. Kama ningalicheza gofu, ningekuwa huko mahali ambako wanawake wako nusu uchi. Na kama ningalikuwa—na kama ningalikuwa mchezaji wa mpira, mnajua vile lingalikuwa, hilo. Lakini nina—nina furaha ilikuwa ni huko nje, kama kuvua samaki, kuwinda na kadhalika.

<sup>2</sup> Nami daima nimethamini moja ya zile bunduki za Weatherby Kubwa. Nami nadhani mtu fulani angalininunulia kama ningalisema jambo fulani kuihusu, bali nilikaa nalo kwa maana ni fedha nyingi sana wanazotaka watu wazinunue, huku nikijua wamishenari hawana viatu miguuni mwao. Halafu nimruhusu mtu fulani ailipie hiyo, achukue kiasi hicho cha fedha na kulipia bunduki? Ndugu Art Wilson alimpa Billy kule nyuma Winchester ya muundo wa sabini si muda mrefu uliopita, Roberts ya miambili-hamsini-na-saba. Bw. Weatherby aliandika kwenye gazeti moja ya kwamba angeweza kuichukua bunduki hiyo aifanyie badiliko kidogo tu mle ndani na kuifanya iwe ni Weatherby Kubwa, ikiwa tu salama kabisa. Kwa hiyo Ndugu Rodney anayekuja hapa kanisani, Ndugu Rodney Armstrong aliituma na akafanya waibadilishe iwe Weatherby Kubwa. Ilitukia tu kwamba haikubadilishwa vizuri. Kwa hiyo wakati nilipoipiga, ni hiyo Weath-...Kampuni ya Winchester inasema ya kwamba bunduki yao itastahimili presha ya ratili elfu sita na mia tisa za kanieneo. Mnajua hiyo ingekuwa ni kitu gani.

<sup>3</sup> Na ilinibidi tu kulenga shabaha, Ndugu Wood alishuka akaenda kule pamoja nami, na ilikuwa tu karibu inchi moja kutoka kwenye jicho langu, namna hiyo. Na presha iliyolipua ratili elfu sita na mia tisa umbali wa yadi hamsini, mtutu wa bunduki ulichomoka ukaelekea kwenye ule mstari wa yadi hamsini, komeo lilirudi nyuma upande huu, na bunduki ikachanguka tu vipandevipande mkononi mwangu. Mwali wa moto tu wenye urefu wa kama kufikia dari lile pale, na hayo ni karibu yote niliyojua kwa sekunde moja ama mbili. Na, nilipojirudia, damu ilikuwa ikibubujika namna *hii* kote, nami niliwazia nilikuwa nimeuawa, kwa hiyo kwa namna fulani niliushika mkono wangu juu namna *hiyo* kwa dakika moja. Na

Ndugu Wood. . . Nilijaribu kuangalia, wala sikuweza kuona kwa jicho hili, wala nisingeweza kusikia hata kidogo. Nilijisikia kana kwamba nilikuwa nikitembea hewani. Basi nikamwona Ndugu Wood akielekea kwenye shabaha akaone mahali ambapo risasi ilipiga, nami nikajaribu kuvutia welekevu wake. Ndipo akafika pale nasi tukaja. Na duara ya marisau ilikuwa moja kwa moja imelizunguka jicho. Na uso wangu ulionekana kana kwamba wakati uo huo yeye alikuwa ameutupia sambusa, ambapo ndio kwanza iulipue uso wangu. Na vipande vikubwa vizito vilikuwa vimepenya juu kidogo tu ya jicho, na kufanya duara moja kwa moja kuzunguka mfupa wa pua na mfupa wa fuvu *hapa*. Daktari Adair alivitoa.

<sup>4</sup> Siku chache baadaye, hasa, kesho yake, Dak alikuwa hospitalini mwenyewe. Walinipeleka kwa mtaalamu kuhusu jicho. Aligundua duara, chini tu ya jicho, ya karibu vipande thelathini vya marisau vilivyopenya moja kwa moja kwenye mboni ya jicho. Haviwezi kutolewa. Viliingia, vikakosa kidogo tu kupenya sehemu ya kuonea na kufanya duara kuizunguka namna hii. Yeye akasema, “Jambo pekee nijualo,” alimwandikia Daktari Adair barua, kasema, “hapana shaka Bwana mwema alikuwa ameketi kwenye benchi pamoja naye, kumlinda mtumishi Wake, la sivyo hata asingekuwa na kichwa kilichosalia juu yake.” Yote ambayo Ndugu Wood angalikuta yangekuwa ni kutoka *hapa* kwenda chini, mnaona. Hiyo presha iliyolipuka kurudi nyuma! Sijui jinsi ilivyofanya hivyo. Lakini komeo hilo kubwa na zito kutoka kwenye bunduki ya muundo wa sabini lilikuwa limelipuliwa likarushwa huko nyuma kabisa, kama unajua mahali Kilabu cha Conservation kilipo, huko nyuma kabisa kwenye zizi la kulungu. Na sehemu ya bunduki hiyo hatukuipata kabisa.

<sup>5</sup> Kwa hiyo, inaonyesha tu jambo fulani. Nina mahubiri siku moja juu ya jambo hilo, Bwana akipenda, juu ya “Wongofu ni sawa, bali afadhali unyenyekee. Kama haujakusudiwa kwa mzigo unaobeba, utalipuka kila wakati.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo usijaribu kuninii. . . Afadhali uwe ni ule wa asili. Sio utani kutoka kwenye baadhi ya. . . [Dada fulani anazungumza kutoka kwenye kusanyiko—Mh.] Sasa angalia, unaona. Ni ninii. . . Loo, hakika, ungeweza kuwazia ya kwamba mambo yangesemwa namna hiyo.

<sup>6</sup> Lakini, nijuavyo mimi, hakuna—hakuna jambo moja. . . Hakika, masikio yangu, unaweza kuwazia, yangali yanalialia wakati maikrofoni hii inarudisha mwangwi. Hiyo ndiyo sababu sikuwa hapa asubuhi ya leo. Ukizungumza, unaisikia ikilipuka tena. Lakini walinipeleka kwa mtaalamu fulani, kasema, “Kiwambo cha sikio hata hakijavimba. Na halafu jicho,” kasema, “utaona tu jinsi ulivyowahi kuona.” Kasema—kasema, “Ilingia chini ya sehemu ya kuonea. Ilifanya tu duara

kuzunguka mboni ya jicho, ikajipenyeza ndani.” Kasema, “Sikuzote utakuwa na marisau.”

<sup>7</sup> Nikasema, “Nimekuwa nayo tangu nilipokuwa na umri wa miaka miwili, hiyo ni kutoka kwenye nyingine.”

<sup>8</sup> Ndugu Roberson kule nyuma, nilimpigia simu na nilikuwa nikimwambia habari zake. Akasema, “Usijali hilo,” kasema, “nina ratili mbili ama tatu ndani yangu,” alisema. Yeye ni shujaa aliyebobea kutoka vitani. “Kwa hiyo haitadhuru, nimekuwa na nyingi kama hizo.”

<sup>9</sup> Nami ninakumbuka ono la Bwana si muda mrefu uliopita. Je! mnakumbuka nikilielezea hapa? Wema wa Bwana asubuhi hiyo, kasema, “Usihofu chochote, popote uendapo, ama lolote, kwa kuwa Uwepo usioshindwa wa Yesu Kristo uko pamoja nawe popote uendapo.” Kwa hiyo hawezi, Shetani hawezi kuniua mpaka Mungu aseme “imekwisha.” Unaona? Huenda akajaribu, bali kamwe hatafanikiwa katika kufanya jambo hilo.

<sup>10</sup> Kwa hiyo basi, jambo la ajabu, nilikuwa nikiendelea hata hivyo, nikienda kwenye mkutano wangu, ambapo ningeweza kuona vema kutoka kwenye jicho hili la kushoto, nami nilikuwa nikienda kwenye mkutano huo kwa vyovyote. Ndipo wao, yule ndugu aliyekuwa akienda kwenye sehemu iliyotengewa Wahindi, ilimbidi kufutulia mbali mkutano huo, ama kuahirisha, mpaka nitakaporudi kwenye Pwani ya Magharibi na kwenda mpaka Pwani ya Magharibi. Kwa hiyo tutaenda kufanya mkutano kule. Na kwenye wakati huu, Ndugu Arganbright amenishikilia, ndipo wakati mkutano huo utakapokwisha, pia nitaenda huko Anchorage, Alaska. Ndiyo sababu nilikuwa nikitumainia sana . . .

<sup>11</sup> Wengi wenu mnakumbuka lile ono nililokuwa nalo, ambapo nilikuwa nimempiga risasi yule dubu mkubwa mkali, dubu wa futi tisa, (na kanisa linakumbuka nikiwaambia hapa), na kuro. Nilikuwa na lingine. Kumbukeni liko kwenye kanda hapa, nilimwona dubu mkubwa mno wa hudhurungi. Huyu huenda akawa ni Kodiaki na huenda isingefanikiwa kule Canada, kwa kuwa hawako kule, mnaona. Lakini hata iwe ni wapi, itakuwa. Itakuwa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Itakuwa. Mnaona?

<sup>12</sup> Na sasa nawashukuru kwa kuniombea. Nilijua wengi wenu mngekuwa mkiomba mliposikia ya kwamba nilikuwa nimeumia. Na kundi moja dogo ambalo linaninii tu . . . Binti yangu kule nyuma, Rebekah, alimwandikia Dada Dauch ambaye huja hapa kanisani, barua, na kumpasha habari hiyo. Ndipo akampigia Meda simu siku chache usiku baada ya hilo, akasema, “Sijui kama lilisaidia ama halikusaidia, bali sisi sote kundi hili hapa tulikutanika.” Yule Mhudumu Mmethodisti na—na Ndugu Brown, jamaa yao na hao wote pamoja walikusanyika, wakaomba usiku kucha kwa ajili yangu. Kasema, “Sijui kama Mungu alisikia ama hakusikia, lakini, tulijua ya kwamba Ndugu

Branham aliwaombea wengi sana, tuliwazia tungemwombea.” Hao ndio aina ya anaowasikia, unaona. Hiyo ni kweli, hao wa namna hiyo!

<sup>13</sup> Ndugu Crase, mmoja wa ndugu zetu hapa, Shetani alimwandama hivi majuzi, aligonga kalvati, loo, ikakata tu ninii yake. . . kabisa. Sioni jinsi alivyowahi kutoka hapo akiwa hai. Na kwa hiyo alikuwa amelala kule hospitalini na akasema kulikuwa na maskini ndugu mmoja aliyekuja kutoka New Albany, jina lake ni Medcalf, naye akasema, “Ndugu Crase, si—si—sistahili kuja kukuombea, lakini,” akasema, “Bwana aliliweka tu moyoni mwangu, kwa hiyo nisingeweza kujizuia. Ndipo akatoka akaja na kupiga magoti, akaomba maombi mafupi kisha akatoka. Mungu alimponya Ndugu Crase papo hapo. Unaona? Wakati, unaona, ni karama ya uponyaji katika Mwili wa Kristo, unaona, mshiriki mmoja kwa mwingine.

<sup>14</sup> Usifikiri ati kwa sababu wewe ni mshiriki wa kawaida tu; ilivyo, wewe ni mshiriki tu kama mtu mwingine yeyote. Hicho ni kidole changu tu kama mkono huu ulivyo mkono wangu, ama sikio hili lilivyo sikio langu. Unaona? Ni mshiriki tu wa mwili. Nasi sote. . . Kama kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote pamoja huumia nacho. Umoja, jinsi ulivyo umoja uliobarikiwa! Sasa mimi. . .

<sup>15</sup> Ndipo baada ya jambo hilo, sasa, nimeendesha mikutano mingine zaidi na kuacha wakati mdogo hapo kwa ajili ya usiku tena pamoja na maskani, Bwana akipenda. Na, Mungu akipenda, Jumapili hii nyingine ijayo asubuhi ninataka kuzungumza juu ya *Nyayo za Nabii*, na halafu, kwenye maskani.

<sup>16</sup> Kesho usiku, ama Jumapili usiku, niko hapa kwenye Maskani ya Injili, mmoja wa ndugu zetu, Ndugu Ruddell. Ninataka kuzungumza juu ya somo, *Kutoa Mvuuke*, Bwana akipenda.

<sup>17</sup> Na halafu Jumanne ijayo, inatubidi kuondoka basi kwenda Wisconsin, kukiweko na mkutano wa Mkoa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Nitakuwa kule kwa siku tatu usiku. Hiyo ni kwenye. . . Billy, mji huo unaitwa jina gani? Nilipokea. . . [Ndugu Billy Paul Branham anasema, “Green Lake.”—Mh.] Green Lake, Wisconsin. [“Alhamisi.”] Lini? [“Alhamisi, Ijumaa, na Jumamosi; tarehe kumi na saba hadi kumi na tisa.”] Alhamisi, Ijumaa, na Jumamosi; tarehe kumi na saba, kumi na nane, na kumi na tisa, huko Green Lake, Wisconsin, mkutano wa mkoa.

<sup>18</sup> Na halafu Jumapili, ya tarehe ishirini, niko Chicago kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya juu, ukumbi ule ule tuliokuwamo wakati wa mwisho. Unakumbuka jina hilo ni lipi? [Ndugu Billy Paul anasema, “Stephen Mather.”—Mh.] Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Juu ya Stephen Mather, kwa ajili ya Jumapili alasiri.

<sup>19</sup> Halafu Jumatatu niko huko ninii... Nasahau jina la mahali hapo ambapo Bwana alinionesha mkutano wakati ule kuhusu Shirika la Wahudumu wa Chicago, wakikutana nami kuhojiana juu ya mada, mwajua. Nilisema, “Na Bwana alinionesha mahali hapo.” Ni mkutano wa kumuaga Ndugu Joseph Boze, ambaye atawasili hapa kesho kwa ndege kuniona mimi, na karamu ya kumuaga Jumatatu.

<sup>20</sup> Halafu tutakuja moja kwa moja nyumbani na kuondoka baada ya hapo, kwa kuwa itakuwa ni wakati basi wa kuondoka kwenda Pines ya Kusini, Carolina ya Kusini, ama Carolina ya Kaskazini. Na halafu kushuka kwenda Columbus, Carolina ya Kusini. Na halafu basi kwenda Cow Palace kwenye Pwani ya Magharibi. Halafu basi kupanda kwenda kupitia Grass City, na mpaka kuingia Spokane, hata Canada, halafu kuingia Alaska. Kwa hiyo iweni katika maombi kwa ajili yetu, kweli tunahitaji maombi yenu.

<sup>21</sup> Nasi tunafundishwa katika Maandiko ya kwamba mambo yote hutenda kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu. Nami ninaamini, kwa kuwa jambo hili, na kwa kuona uaminifu wa watu na kadhalika... Mtu fulani alisema, “Ingetendekaje, na kwa nini Mungu angeiruhusu?” Ningaliuawa barabarani nikienda huko, kitu kama hicho ama kinginecho, Yeye—Yeye alikuwa na kitu cha kuliepa hilo. Kumbukeni, Maandiko hayawezi kukosea, “Mambo yote hutenda kazi pamoja kwa manufaa ya wale wanaompenda Mungu.” Na, kama ninaujua moyo wangu, ninampenda. Ni—ninampenda kwa moyo wangu wote. Nalo linatuleta karibu zaidi pamoja.

<sup>22</sup> Na, kuwazia sasa, ya kwamba kila mtu ambaye amesikia hilo, hawezi kuelewa jinsi ambavyo nina kichwa ama mabega yaliyosalia, mnaona, nami nikiketi kwenye mlipuko huo wote. Hilo, karibu *hivi* na mimi, ambao labda ungekuwa ni mlipuko wa karibu ratili elfu mbili moja kwa moja usoni mwako. Unaona, huo unatosha tu kukuchangua vipandevipande, unaona, kukufagilia tu mbali. Kama uliivunja bunduki hiyo nzito ya feleji na kulipua mtutu huo moja kwa moja kuelekea kwenye ule mstari wa yadi hamsini, na—na tako, laiti ungaliiona bunduki hiyo. Kamwe haionekani kama bunduki, ni vipandevipande tu vilivyookotwa.

<sup>23</sup> Halafu basi, kutokana na jambo hilo, bila ya dosari hata moja. Asifiwe Mungu aliye hai! Ya kutosha tu kunifanya nisiende kule mpaka lile neno kutoka kwa Eddie lilipokuja ya kwamba sikupaswa kuja kwenye wakati huo. “Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika kuwa tamu, iliyomwoko mwovu kama mimi!” Na inatufanya tujue ya kwamba, kumthamini Mungu akiwa pamoja na sisi. Mungu yu pamoja nasi, na jinsi tunavyoshukuru!

<sup>24</sup> Sasa, niliwaambia asubuhi ya leo nilidhani nitashuka nije huku, ndipo ndugu mpenzi hapa niliporudi... Nilimwambia

Dada Wood leo, nadhani Ndugu Neville. . . Billy alinipigia simu na kusema, “Usikilize ujumbe huo ukiweza.” Nami ninaamini kipande kidogo cha chuma hicho kilikuwa kimejipenyeza chini ya jicho langu pale, kwa kweli kilikuwa kikinipa shida kusafiri, bali sasa kimetolewa. Walikiosha kikatoka. Na kwa hiyo basi akasema. . . Usiku huu nilifikiri ningeshuka kwenda huko, na huyo ndugu wa thamani labda akihubiri namna hiyo, ninajua ni kitu gani wakati una ibada moja kubwa kisha unapwelewa sana na sauti, unajua, na—na koo likiwaka na kuuma. Kwa hiyo nilifikiri nitashuka niende kule, na nikachukua Maandiko machache ya kusoma. Nikawazia, “Usiku wa ushirika.”

Daima ninataka kula ushirika.

<sup>25</sup> Basi nilikuwa na marafiki kadhaa, wako hapa mahali fulani. Sioni vizuri sana, kama mnavyofahamu. Kungali kuna belladonna ndani ya jicho hilo ambalo limevimba, kwa namna fulani lina ukungu. Na kwa hiyo wako hapa, marafiki na jamaa za ndugu yangu mpendwa wa thamani, F. F. Bosworth, aliye Utukufuni. Kwa hiyo Bwana na awabariki watu hao, ndiyo kwanza tuwaombe katika chumba cha huko nyuma.

<sup>26</sup> Sasa, msisahau, Jumatano usiku ndio mkutano wetu wa maombi ya katikati ya juma. Nami nafikiri, Ndugu Jackson, wake ni Alhamisi usiku. Na Ndugu Junior hapa juu ni. . . Ama, Ndugu Ruddell ni Jumatano usiku. Na maskani ya Utica ni Jumatano. [Ndugu Neville anasema, “Huo uko Alhamisi usiku.”—Mh.] Alhamisi usiku. Halafu tutarudi hapa Jumapili asubuhi kwa ajili ya ibada ya kusanyiko.

<sup>27</sup> Halafu basi sasa, na Jumapili usiku sina budi kuwa pamoja na Ndugu Ruddell. Nilikuwa nilifanye hilo Jumatano usiku, lakini juma lijalo, lakini siwezi kufanya hivyo, kwa hiyo ilinibidi kuliweka hilo Jumapili usiku. Lakini sasa watu hapa maskanini, kaeni papa hapa maskanini, mnaona, maana nitaenda kwa Ndugu Ruddell usiku huo kuhubiri tu, si kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Na, lakini kumbukeni, kaeni hasa kwenye wajibu wenu, papa hapa maskanini. Hapa ndipo mahali penu, mnaona. Na kwa hiyo tutatarajia wakati mzuri. Na basi nyote mtuombe tunaposafiri.

<sup>28</sup> Tunatumaini ya kwamba Mungu atakutana nasi usiku wa leo sasa kabla tu ya ushirika. Na sasa nafikiri. . . Je! hayo ndiyo yote tuliyoyayo, matangazo, tunayojua? [Ndugu Neville anasema, “Naam.”—Mh.] Sasa, tukiandaa njia. . . [“Mazishi, kesho alasiri.”] Ati nini, ndugu? [“Mazishi, kesho alasiri, saa nane.”] Mazishi. [“Huko Edmonton. Mama wa J.T.”] Loo, naam. Mazishi ya. . . mmoja wa ndugu zetu wainjilisti kutoka kwenye maskani hii hapa ana ninii tu. . . Vema, yeye ni mmoja wetu hapa. Yeye hutoka anaenda kuhudumu na kuhubiri, Ndugu J. T. Parnell. Maskini mama yake wa thamani alikufa hivi majuzi usiku, mama mdogo, aliyeinama, mwenye mvi. Na hayo

yatakuwa huko Edmonton, Kentucky. Ibada ya mazishi ni kesho. Ninajua wengi wenu mlishangaa, mngeweza kumpelekea maua, bali sisi tusingeweza. Na njia pekee kanisa lilivyopeleka shada kule, iliwabidi kupiga simu halafu mtu wa posta akalipeleka. Na ingebidi yatumwe kesho, yafike yasifike kule, maua, kwa hiyo inalifanya kuwa gumu. Lakini hakika tunataka kutuma rambirambi zetu, ndugu, kwa Ndugu yetu Parnell kumpoteza mama yake, jambo ambalo, nimefanya vivyo hivyo hivi karibuni tu. Nami nina hakika ya kwamba Dada Spencer na wengine wengi hapa ambao wanatuma rambirambi zao, pia, ambao hivi karibuni walipitia kwenye vivuli na huzuni.

<sup>29</sup> Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, katika Uwepo Wake, kwa maombi. Sasa nawatakeni mniombe. Na kwa namna fulani ni vigumu hapa usiku wa leo, kujaribu kuona, na taa hii ikiniumiza macho. Na—na jicho langu ni sawa, bali walilitia belladonna kidogo lipate kuvimba. Mnajua ni kitu gani. Na limekuwa hivyo kwa yapata siku sita sasa, unaona, naye alisema huenda ikachukua juma lingine ama siku kumi. Kwa hiyo niombeeni. Halafu mwangwi kutoka kwenye maikrofoni hii unaotoka kwenye hizi kuta, niombeeni. Nami ningeweza kuuona mkono wako, na Mungu, ukiwa na haja inua tu mkono wako. Mungu, yajibu maombi, tunapokusanyika kwa uchaji na kuinama sasa.

<sup>30</sup> Baba yetu wa Mbinguni, Wewe umechagua ya kwamba inatupasa kukusanyika pamoja. Ni mapenzi ya Mungu ya kwamba inatupasa kukusanyika pamoja tunapooona ile Siku ikikaribia, na hiyo ni mara kwa mara, Bwana, kujileta wenyewe karibu zaidi na Wewe na karibu zaidi mmoja kwa mwingine, katika kifungo cha ushirika, kupitia Damu iliyomwagika ya Yesu ambayo inafanya jambo hilo liwezekane.

<sup>31</sup> Tunashukuru sana usiku wa leo, Bwana. Si—si—sijapata kuwa na shukrani sana ku—kuwa hapa, Bwana. Mimi, ninakushukuru sana. Siwezi kamwe kupata maneno ya kueleza jinsi nilivyo na shukrani kuwa na macho na kusikia, na kuwa miongoni mwa walio hai hapa duniani, kuiendeleza Injili. Linatufanya tuwe na shukrani sana, Bwana, tunapooona jinsi tu hiyo ilivyo karibu... Wakati watu wenye akili sana wanapokuna tu vichwa vyao na kusema, “Ingewezekekanaje? Ni mkono wa Mungu tu!” Ndipo ninainamisha kichwa changu kwa unyenyekevu, Bwana, kuona ya kwamba muujiza huo nilipewa mimi, kwamba ufanywe karibu na mahali ambapo mtumishi Wako alikuwa amesimama. Ninashukuru sana. Na sasa, Baba, ninayaweka wakfu upya maisha yangu katika utumishi Wako tena, baada ya kushuka kwenda kule. Kamwe mtu hawezi kuwa karibu zaidi na mauti maishani kuliko wakati huo, na kisha aishi. Kwa hiyo ninashukuru.

<sup>32</sup> Na sasa ninawaombea watu hawa wote ambao waliinua mikono yao usiku wa leo, kila mmoja wao alikuwa na haja.

Na wengi wao wanatoa shukrani, karibu wote, Bwana, mioyoni mwao, kwa yale uliyowafanyia pia.

<sup>33</sup> Sasa tumekuja usiku wa leo kukusanyika katika wakati maalumu sana, hiyo ni kusema, kula tunachoita “ushirika,” ama, “Meza ya Bwana.” *Kushiriki* ni “kuongea na, ama kuzungumza na.” Na hivyo ndivyo tunavyofanya sasa, Bwana, kuzungumza na Bwana wetu, kushiriki, kuzungumza, tukimngoja Yeye atupe jibu Lake.

<sup>34</sup> Na sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utasema nasi usiku wa leo kwa Neno lililoandikwa. Na utupe kitu fulani mioyoni mwetu, kuimarisha safari ye—ye—yetu, Bwana, na kutupa ujasiri mpya. Na umbariki mchungaji wetu, Bwana, ndugu yetu wa thamani, mtumishi Wako, na mke wake na familia; na mashemasi na wadhamini, na kila mtu anayekuja kanisani. Ee Mungu, tusogeze karibu na Wewe. Jalia kuwe, kama vile mshairi alivyosema, “Kibarikiwe kifungo kiifungacho mioyo yetu katika upendo wa Kikristo. Ushirika wetu wa watu wenye nia moja ni kama wa huko juu.” Tujalie, Bwana. Wabariki waabuduo wengine wote kote ulimwenguni. Na sasa, Baba, tuvunjie Mkate wa Uzima tunapokungojea Wewe. Katika Jina la Yesu Kristo, Mtoto Wako mpendwa, tunaomba. Amina.

<sup>35</sup> Sasa, watu wengi wanapenda kuandika maneno ambapo huenda mhudumu akapasoma. Nami nina... Alasiri ya leo baada ya mimi kutoka pamoja na Ndugu na Dada Wood... Tulikuwa huko chini kumwona Ndugu yetu Gobel Roberson, na kwa hiyo tulikuwa, katika chumba chake cha maonyesho. Kwa hiyo tukarudi, nami nikafikiri... Dada Wood alikuwa akiniamba ni ujumbe mzuri jinsi gani ambao mchungaji wetu alikuwa nao asubuhi ya leo. Nami ilitokea tu kwamba niliwazia juu ya maskini jamaa huyo, labda amepwelewa na sauti, nami nimepwelewa pia, lakini ni—nilifikiri tungeweza kushiriki hili pamoja, labda, kama akiniomba nizungumze. Nami niliandika mihtasari michache hapa ambayo ningetaka kuzungumzia.

<sup>36</sup> Kwanza, hebu tufungue Wakorintho wa Pili 6:7 hadi 10. Wakorintho Wa Kwanza, mlango wa 6, kifungu cha 7 na cha 10, vyote pamoja. Halafu Mwanzo 14:18 hadi 19. Na tutoe kutoka hapo, Bwana akipenda, mukt-... ama muktadha kutoka kwenye fungu hilo. Na sasa nitasoma kutoka ninii wa Kwanza... ama kutoka Wakorintho wa Pili, wa kwanza, Wakorintho wa Pili 6:7 hadi 10.

*Katika neno la kweli, katika nguvu ya Mungu; kwa silaha za haki, za mkono wa kuume na za mkono wa kushoto;*

*Kwa utukufu... aibu; na kwa kunenwa vibaya na kunenwa vema; kama wadanganyao, bali ni watu wa kweli;*

*Kama wasiojulikana, . . . bali wajulikanao sana; kama wanaokufa, kumbe tu hai; kama wanaorudiwa, bali wasiouawa;*

*Kama wenye huzuni, bali sikuzote tu wenye furaha; kama maskini, bali tukitajirisha wengi; na kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote.*

Mwanzo 14:18 na 19.

*Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa aliye juu sana . . .*

*Akambariki Ibrahimu, akasema, Ibrahimu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi:*

<sup>37</sup> Na kama ningeliita fungu la maneno, ningetaka kuzungumza juu ya somo, la . . . *Kumiliki Vitu Vyote*. Kama vile katika Wakorintho hapa, sisi . . . Ilisema ya kwamba sisi ni—ni maskini, bali tu wenye vitu vyote. *Kumiliki Vitu Vyote*. Sasa, ninapenda hilo. Sasa katika Mwanzo tunasoma juu ya Ibrahimu akikutana na mtu huyu mkuu anayeitwa Melkizedeki, ambaye alikuwa Muumba wa Mbingu na nchi pia. Halafu, Yeye alikuwa ni Mwenye vitu vyote, Muumba wa Mbingu na nchi, hilo ni kusema, vitu vyote.

<sup>38</sup> Sasa, tunajua hadithi ya Ibrahimu na yale yaliyokuwa yametukia. Yeye alikuwa ameitwa aende ma—mahali pa wajibu. Alikuwa ameitwa atoke kwenye nchi yake, nchi ya Wakaldayo, na mji wa Uru, ambako alikuwa kule pamoja na baba yake na watu wake. Na huko ndiko kwenye mabonde ya Shinari, labda nchi tajiri yenye rotuba. Naye Ibrahimu, tunavyofahamu, hakuwa mtu yeyote maalumu machoni pa ulimwengu. Na hata hivyo, hakuwa mfalme, ama mtawala, ama mtu mkuu. Yeye alikuwa ni mtu tu. Naye alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, ambaye alikuwa ni Sara, na pengine alimwoa wakati alipokuwa msichana. Na Mungu alikuwa amemwita kwenye umri wa miaka sabini na mitano, kwa maisha ya utumishi, na ilikuwa ni pamoja na msaidizi wake pia.

<sup>39</sup> Na papa hapa tungeweza kuanza. Ninaamini ya kwamba wakati Mungu anapomwita mwanamume kwenye huduma, kama yeye ni mtu aliyeoa na ana msaidizi, Yeye humwita mke wake pamoja naye, kwa sababu hao wawili ni mmoja. Na kwa hiyo, popote, tunaona baadaye kidogo ya kwamba labda Mungu angeweza kumwua Sara wakati aliposhuku ule ujumbe wa Malaika, miaka ishirini na mitano baadaye, wakati walipokuwa wameketi chini ya mwaloni siku ile, lakini wakati alipocheka wakati yule Malaika alipomwambia, ama alipomwambia Ibrahimu ya kwamba atakuwa mjamzito, ndipo Sara akacheka moyoni mwake na kusema, “Ningewezaje mimi, mkongwe?” Umri wa miaka tisini, na mumewe umri wa miaka mia moja. Ninii yake . . . tumbo lake la uzazi lilikuwa limekauka

kwa miaka kadhaa, na mwili wa mumewe ulikuwa kama mfu. Basi angeweza kamwe kuwa na raha na mumewe tena? Ndipo akacheka moyoni mwake.

<sup>40</sup> Naye Malaika, akiwa ameelekeza mgongo wake hemani, alisema, “Kwa nini Sara akacheka?”

<sup>41</sup> Naye akakanusha jambo hilo. Sasa, hilo ni kumwambia Mungu usoni Mwake ya kwamba Yeye “amekosea.” Unaona? Na hilo lingaliuondoa uhai wake, lakini Mungu asingeweza kumwondoa Sara, kwa sababu yeye alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Unaona? Naye alikuwa katika agano pamoja naye, kwa hiyo ilimbidi kuambatana naye. Kwa hiyo Yeye asingeweza kumwua Ibrahimu... ama kumwua Sara, pasipo kuiondoa sehemu ya Ibrahimu, kwa kuwa hawa wawili ni mmoja.

<sup>42</sup> Mfano mzuri wa sisi leo, tusiostahili, tunaostahili kifo tunapotenda dhambi, bali Mungu hawezi kutuua, kwa kuwa Yeye angeninii... sisi ni sehemu ya Kristo. Unaona? Hiyo ni neema yetu, kwa sababu tumeunganishwa na Kristo. Hilo si ni wazo linalopendeza, kuunganishwa na Kristo? Kwa hiyo basi, dhambi zetu, tunapozitenda, tunapaswa kuzikiri haraka, ya kwamba “ni makosa,” kwa kuwa Mungu angeutwaa uhai wetu. Bali Damu inajibu kwa niaba yetu, wala Mungu hawezi kamwe kuivuka hiyo Damu. Unaona? Kamwe hawezi kufanya hivyo, kwa maana ni ahadi ya kwamba hatafanya hivyo. Kwa hiyo hawezi kuvunja ahadi Yake Mwenyewe. Unaona? Kwa hiyo Mungu, kwa kweli, amejifunga kabisa. Unaona, hawezi kuvunja ahadi Yake. Naye aliahidi jambo hilo kupitia hiyo Damu, yeyote aliyeamini alikuwa na Uzima wa Milele, wala Yeye hawezi kuvunja ahadi hiyo.

<sup>43</sup> Kwa hiyo tunaona ya kwamba Ibrahimu, katika kutii, aliyaacha makazi yake, akaacha ardhi yake, na kujitenga na kila kitu, hadhi yake yote ya duniani, mali, apate kusafiri katika nchi ya kigeni, akiwa mgeni. Mfano wa Kanisa. Tunaalikwa kuacha kila kitu kilichomo humu ulimwenguni, kusudi tumfuate Kristo.

<sup>44</sup> Sasa, tunamwona Ibrahimu akiendelea, mwaka baada ya mwaka. Naye akachukua sehemu fulani kuambatana naye, ambayo ilikuwa ni baba yake, naye akafa mara moja. Na kisha akamchukua binamu yake, ambaye alikuwa ni Lutu, naye Lutu akajitenga kutokana na mabishano, akashuka akaenda kuishi Sodoma, hata hivyo alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Na Mungu akaitoa hiyo nchi na yote yaliyokuwa katika nchi hiyo, akampa Ibrahimu, akairithi yote. Mungu akasema, “Angalia mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, na yote ni mali yako na uzao wako baada yako. Yote ni yako!”

<sup>45</sup> Sasa, siku moja Ibrahimu alikuwa na wakati mgumu, naye Lutu akiwa na maisha ya raha, akigaagaa katika dhambi. Jinsi ilivyo rahisi na jinsi dhambi inavyoonekana ni tamu, na jinsi inavyoonekana isiyo na hatia. Sasa, kama Lutu akisema hivi,

“Mradi tu ninaamini! Ninamwamini Mungu, kwa hiyo mbona nishuke niende hapa Sodoma, na—na itakuwa ni sawa. Mimi ni mwaminio.” Lakini haikuwa ni sawa.

<sup>46</sup> Mnaona, Mungu, wakati alipomwita Ibrahimu, Yeye alimwita apate kujitenga na kila kitu. Na hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya. Mungu anaita kwenye kujitenga kabisa na dhambi, “Tokeni kati yake, msiishiriki!” Jitengeni nayo, mwonekano wa uovu wenyewe. Kujitenga, kuondolewa kwake kabisa! Kaeni mbali sana nayo. Msikanyage ardhi yake, hata iwe—iwe. . . inaonekana nzuri jinsi gani.

<sup>47</sup> Ninyi watu, huenda mkafikiri hapa sasa, ni hivi, “Ndugu Branham, mimi—mimi wakati mwingine ninashawishika kuiba, ama wakati mwingine ninashawishika kuvuta sigara.” Ama wakati mwingine wanawake wanafikiri, “Ninashawishika kuvaa kama watu wa ulimwengu, unajua, nguo chafu na kadhalika. Ninashawishika,” wasichana. Sasa, unafikiri hilo ni la kutamanisha, vipi kuhusu huku ambako inakubidi kuangalia kila hatua ndogo, unaona, katika huduma. Ni jambo kubwa zaidi jinsi gani huku, na jinsi ambayo itawabidi kuwajibika kwa wingi zaidi. Kwa sababu, itawabidi kuwajibika kwa nafsi zenu wenyewe, bali inatubidi kuwajibika kwa kila mtu tunayezungumza naye. Unaona? Kwa hiyo Shetani daima tu. . . Vema, unasema, “Hivi hiyo si ni nguo fupi inayopendeza? Ni vibaya kabisa kuvaa, lakini si inapendeza? Ingenikaa vizuri kabisa.” Ambapo kwangu mimi. . . Sasa, hilo, wewe unajua hilo ni kosa. Lakini kwa mhudumu ni, “Unapaswa kwenda kwenye mkutano huu hapa, huu ndio wenyewe. Wanasema ni kubwa sana, kusanyiko hilo.” Na hata hivyo inakupasa kungojea na kumsikia Mungu akisema, “nenda,” unaona. “Loo, je! ungeweza kwenda huku na kumwona mtu huyu hapa? Huyu ni *nanii*.” Na inakupasa kuangalia, kuwa mwangalifu. Unaona? Loo, ni janja sana. Na sasa inatupasa kuangalia mambo hayo.

<sup>48</sup> Sasa, ilimbidi Ibrahimu kuangalia, pia. Lakini yeye, badala ya kushuka kwenda Sodoma pamoja na Lutu, alijitenga mwenyewe na akapanda kwenda jangwani, akaambatana na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Huo unapaswa kuwa ndio msimamo wetu. Ambatana na watu wa Mungu haidhuru kama ni ngumu ama ni rahisi, nenda hata hivyo. Kuwa tayari kwenda wakati wowote, sasa, popote Yeye angekuita.

<sup>49</sup> Sasa, baada ya jambo hili kuzuka, ndipo a—akaja mfalme aliyeenda kupigana na kabila dogo la watu kule juu, na akalivamia hilo bonde na kuyateka makundi hayo yote madogo, falme ndogo angeziteka, na akauteka, akaingia Sodoma na kumchukua mateka mfalme wa Sodoma na Gomora, akamteka Lutu (binamu wa Ibrahimu), mke wake, binti zake, watoto wake, wote hao, na mali yao yote, yote waliyokuwa nayo, na akapita moja kwa moja, akaenda akiifagia nchi. Loo, ni jambo la kuchukiza jinsi gani, mshahara wa dhambi ni mauti! Lutu

alitambua, hapana shaka, akitembea pale na labda akiwa na ka—kamba ama mnyororo shingoni mwake, kama mtumwa; watoto wake, wasichana wakabakwe; na mke wake, na kila kitu, na labda afe wakati wowote. Alikaidi amri moja, na labda akienda kwenye ufalme mwingine mahali fulani akafanywe mtumwa siku zake zilizosalia.

<sup>50</sup> Lakini Ibrahimu, wakati alipoona ya kwamba Lutu alikuwa amechukuliwa, hiyo ilikuwa ni sehemu ya urithi wa Ibrahimu. Na huenda ikawa Ibrahimu alisema hivi, “Mungu, uliniambia ya kwamba kama ningekutii na kutembea humu, katika nchi hii, Wewe ungenipa hii. Ni mali yangu. Na Lutu ni sehemu ya hii, nami ninaenda kumtafuta.” Kwa hiyo akaweka walinzi, ama akakusanya watumishi wake pamoja, na kuwapa silaha. Basi akawachukua watumishi wake, na akatoka mpaka akawafuata na kumpata mfalme huyu pamoja na falme hizi zingine zote ndogo. Angalia jinsi walivyokuwa ni jeshi kubwa wakati huo basi! Lakini chini ya uongozi wa Mungu, Jemadari Mkuu, alijitenga mwenyewe, akawavamia na kuwapiga wafalme hao, kisha akamrudisha Lutu na falme hizo zote ndogo, akawarudishia hao, kwenye nchi ya uenyeji wao tena.

<sup>51</sup> Ni picha ya jinsi gani ya Kristo katika Ibrahimu pale, akija baada ya adui kuteka kila kitu, na Kristo akaja na kuturudisha tena.

<sup>52</sup> Sasa tunaona katika hadithi hii kuu ya kwamba Ibrahimu, akiwa njiani akirudi, akirudi baada ya kupata ushindi, alikutana na Muumba wa Mbingu na nchi, Melkizedeki, ambaye ni Mfalme wa Yerusalemu, Mfalme wa Salemu, ambao ulikuwa ni Yerusalemu, ambaye ni Mfalme wa Amani, ambaye ni Mfalme wa Haki. Hakuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wala kamwe hatakuwa na mwisho, kwa hiyo huyo hakuwa kitu kingine ila Mwenyezi. Naye alikutana Naye alipokuwa akirudi nyumbani, kutoka kumpiga mfalme. Alikutana na Muumba, Yule Ambaye alimiliki vitu vyote alikutana naye alipokuwa akirudi. Ni jambo lenye utukufu jinsi gani! Sasa Ibrahimu . . .

<sup>53</sup> Ninapenda jambo hili. Ibrahimu alikuwa ni mrithi wa yote, kwa ahadi, kwa hiyo angeweza kudai kila kitu kilichokuwa nchini, na nchi yenyewe. Ibrahimu alikuwa amepewa ahadi. Sasa, tunafahamu ya kwamba Ibrahimu alikuwa maskini kuliko wote nchini mwote, kwa kuwa aliishi huko jangwani, naye aliishi akiwa na amani na Mungu. Naye Lutu, tajiri, aliishi jijini na akawa gavana wa jiji hilo; alikaa langoni, alikuwa ni hakimu, na aliamua kesi za jiji hilo, naye alikuwa na utajiri wote na kadhalika. Lakini Ibrahimu alikuwa huko jangwani, na ninii . . . labda mtu aliye maskini kuliko wote nchini, na hata hivyo alidai kumiliki vyote. Amina! Hilo ndilo ninalopenda.

<sup>54</sup> Loo, usiku wa leo, huenda tusiwe matajiri katika mali ya ulimwengu huu, bali tunamiliki vitu vyote. Kanisa, Lenyewe, linamiliki vitu vyote. Hata ingawa ni maskini, bali ni tajiri na linamiliki vitu vyote. Ninapenda jambo hilo. Yeye. . . Tu—tunamiliki. Ule wimbo wa zamani tuliozoea kuimba miaka kadhaa iliyopita, “Baba yangu ni tajiri wa nyumba na mashamba, Yeye anaushikilia utajiri wa ulimwengu mkononi Mwake! Rubi na almasi, na fedha na dhahabu, makasha Yake yamejaa, Yeye ana utajiri usiosemekana.” Nasi tunazimiliki, kwa maana sisi ni mtoto wa Mfalme. Amina. Mtoto daima huwa mrithi, tunajua. Vema.

<sup>55</sup> Ibrahimu angeweza kushikilia jambo hilo, ingawa ni maskini, ng’ombe wake walikuwa wakifa kwa njaa; Lutu alichukua ardhi iliyokuwa nzuri sana. Maji yake yalikuwa haba. Siku zenye joto, na wachungaji wake walikuwa na shida, na kila kitu kilionekana kimemwendea Ibrahimu vibaya, hata hivyo yeye alimiliki mali hiyo yote.

<sup>56</sup> Na, leo hii, mwaminio wa kweli ametupwa nje kutoka miongoni mwa watu, akaitwa “mlokole, mtakatifu anayejifingirisha,” ama namna fulani ya jina la matusi, namna fulani ya mkereketwa wa kidini, na hata hivyo yeye ni mrithi wa Mbingu zote na nchi. “Heri wenye upole, hao watairithi nchi.” Loo, jamani! Nena kuhusu kukusuma nje kwenye kibanda ama mahali fulani, bila hata pesa za kutosha kulipia kodi yako ya nyumba, hata hivyo unamiliki vyote. Amina. Inakubidi kufanya kazi kwa nguvu na sulubu na kutoa jasho kwa ajili ya dola chache, kupata riziki. . . maisha ya uaminifu, kuivalisha miguu ya watoto wako viatu, na kuulisha mdomo wao mdogo wenye njaa, na hata hivyo unamiliki, ni mrithi wa kila kitu kilicho hapa. “Wenye upole watairithi nchi.” Wanaimiliki. Loo, jamani, ninapenda jambo hilo! Mmiliki wa nchi! Ni kitu gani? Mwaminio. Mwaminio ana hati ya kumiliki, hatimiliki asilia, hiyo ni kweli, kwa Yesu Kristo, ya kwamba “Yeye atakuwa mmiliki wa ulimwengu huu wote.” Hiyo ni kweli. “Wenye upole watairithi nchi.”

<sup>57</sup> Ibrahimu alikuwa—alikuwa, angeweza kumiliki nchi hiyo, kwa sababu. . . na yaliyokuwemo. Mungu alimpa. Na Lutu alikuwa ni sehemu ya nchi hiyo. Kwa hiyo Ibrahimu alikuwa na haki kwa hiyo. Angeweza—angeita ama kuishika. Yeye alisema, “Sasa, Mungu, Wewe ulinipa ahadi, ya kwamba kile kilichokuwa nchi hii na vyote vilivyo ndani yake vilikuwa ni vyangu, Nawe ulifanya ahadi hiyo. Sasa jamaa yangu amechukuliwa, na yote aliyo nayo yameenda.”

<sup>58</sup> Kwa maneno mengine, kama ningaliweza kulitumia kwa siku hizi, ningesema, Kanisa lingeweza kusema, “Bwana Mungu, huyu hapa ndugu yangu, yeye amelala hapa, ameshikwa na kansa, ameshikwa na kifua kikuu, ana *ninii*. Ninaishikilia ile ahadi, ni mali yangu. Wewe, Wewe umeniambia hivyo!” Amina!

Haya basi. Ndipo, ndipo unaweza kumfuatilia adui huyo, ibilisi huyo, na kumpiga kama tu vile Ibrahimu alivyowapiga wale wafalme na kuurudisha urithi wake. Amina. Ninapenda jambo hilo. Ni kwa mwaminio.

<sup>59</sup> Tena Ibrahimu alikuwa na haki kwa ile ahadi, na ahadi hiyo ilikuwa ni yake, hata hivyo ilimbidi kupigana apate kuimiliki. Amina. Haya basi. Mwaminio siku hizi, sasa hivi sisi ni warithi wa vitu vyote, sasa hivi sisi ni warithi wa kila baraka ya kiroho, kila baraka ya kimwili, kila baraka Biblia inayoahidi, hata hivyo inakubidi kupigania kila inchi yake. Hiyo ndiyo jinsi Mungu ameliweka. Sikuzote imekuwa hivyo. Inakubidi kupigana upate kumiliki ile unayojua ni mali yako. Inakubidi kupigana upate kuimiliki. Na hiyo ndiyo inayotupasa kufanya sasa.

<sup>60</sup> Unasema, “Ndugu Branham, ninahitaji uponyaji.”

<sup>61</sup> Ahadi ni yako. Lakini, kama ukiwahi kuipata, hutaipata kwa urahisi, nitakwambia jambo hilo. Itakubidi kuichukua kutoka kwa Shetani. Shetani anakunyang’anya afya yako, una haki ya ku—kumwendea Shetani, useme, “Nirudishie! Irudishe! Ninakuja katika Jina la Bwana, Muumba wa Mbingu na nchi, na mimi ni mrithi Wake. Nirudishie! Ulimchukua mtoto wangu, ulimchanganya na mvulana mbaya. Ulimchukua mvulana wangu na kumchanganya na msichana mwovu. Ninawadai! Hiyo ni kweli. Ninawadai watoto wangu, ninamdai ndugu yangu, ninamdai dada yangu. Naam, Shetani, umewachukua kutoka katika nyumba ya Mungu, ukawashawishi watoke huko, bali ninakuja kuwachukua. Ninawadai.”

“Vema, unajuaje?”

<sup>62</sup> “Mimi ni mrithi wa vitu vyote. Amina. Nimepewa mimi. Mimi ni mrithi, ninaweza kudai kila kitu ambacho Mungu aliniahidi,” Amina. Haya basi. “Ni changu.” Unakipataje, jambo fulani ulilofanya? La, bwana. Ni tuzo tusilostahili ambalo Mungu alitupa, na ni letu, ni mali yetu. Shetani hawezi kulishikilia kama ukimwendea katika Ne—Neno lenye mamlaka la Kimaandiko, pamoja na imani, kusema, “Ni yangu! Iweke chini.” Amina. Utukufu! Ninapenda jambo hilo. “Shetani, iweke chini. Ulininyang’anya. Irudishe, kwa maana ninakupa notisi. Ninayo notisi imeandikwa hapa kwenye Neno, ‘Mbingu na nchi zitapita, bali notisi hii haitapita.’ Kwa hiyo ninakuja na notisi hii, kukupa wewe, ya kwamba Yesu Kristo alisema lolote nitakalomwomba Baba katika Jina Lake atanipa. Nikiuambia mlima huu, ‘ng’oka,’ wala nisitie shaka moyoni mwangu, bali niamini ya kwamba yale niliyosema yatatimia, yatakuwa yangu. Iweke chini!” Hilo linamfanya aanze kuondoka. Si kumfanya aanze kuondoka, kumfanya kutimua mbio. “Iweke chini, kwa kuwa nimekuja kwa mamlaka ya Kimaandiko. Mimi ni mwaminio.” Mnalipata? Naam, bwana. Naam, bwana.

<sup>63</sup> Ilimbidi kufanya nini kwanza, Ibrahimu, kusudi afanye jambo hili? Ilimbidi kuweka imani yake juu ya msingi wa mwamba imara wa Neno la Mungu lililoahidiwa. Angalia, kitu pekee alichokuwa nacho kilikuwa ni kundi dogo la watumishi, pengine dazani moja. Na labda kulikuwa na maelfu kadhaa ya watu, wenye silaha. Na watu wake hawakuwa askari, walikuwa ni watumishi, wachunga ng'ombe, watu wa kondoo, wachungaji; pengine visu vilivyochakaa na vilivyoingia kutu ambavyo walikuwa wameviokota mahali fulani, na kuviweka kwenye... huko nje, na mvua kadhaa zilikuwa zimevinyeshea, vilikuwa vimeingia kutu. Bali Ibrahimu hakuwa akiangalia kisu kilichoingia kutu, ama kutokuwa na ngao hata kidogo. Yeye alikuwa akiweka imani yake juu ya Neno la Mungu. Haya basi. Hilo ndilo linalofanya jambo hilo. Hilo ndilo.

“Utapiganaje nao utakapofika kule?”

<sup>64</sup> “Hilo si juu yangu. Ni juu yangu kuweka imani yangu juu ya yale Mungu aliyosema. Ni yangu, ninafuatilia kile kilicho changu.” Amina. Sasa, wakati watu walio wagonjwa wanapoweza kuona jambo hilo, ugonjwa uko karibu kwisha papo hapo. Unaona? Hakika.

<sup>65</sup> Wakati mwenye dhambi anapoweza kuona ya kwamba haikubidi kutenda dhambi! Watu wengi, wanatenda dhambi kwa sababu inawabidi kutenda dhambi. Hiyo ni hali ya kusikitisha wakati unaposema “yanibidi kutenda dhambi.” Lakini wakati unapotambua kwamba haikulazimu kutenda dhambi tena! Wapo watu ambao wanasimama tu na kulaani na kukucheka usoni mwako, na—na kukuita “mjinga” na chochote kile, hao ni watenda dhambi makusudi. Unaona, basi hakuna tumaini kwao. Lakini mtu yule ambaye anaendelea kufanya jambo fulani, hawataki kulifanya. Yeye—yeye anaiba, hataki kuiba. Pia anasema uongo, hataki kufanya hivyo. A—anafanya mambo a—asiyotaka kufanya, hataki kuwa mwenye dhambi. Kuna matumaini kwake kama unaweza kumwacha aone Ukweli. Unaona? Njoo kwenye ahadi ya Mungu na uweke imani yako juu ya jambo hilo, na utoke uende kule kwa adui. Hawezi kamwe kulishikilia tena, ni hayo tu, kwa sababu ni yako.

<sup>66</sup> Sasa, hebu tumwangelie jamaa huyu sasa. Hapa Ibrahimu alisema, “Mimi ni mrithi. Hii ni mali yangu, kila kitu katika nchi hii ni changu. Kwa sababu Mungu... Sijaipata bado.” Lakini alikuwa anayo, ilikuwa ni yake, kwa vyo vyote vile.

<sup>67</sup> Sasa sisi ni warithi wa vitu vyote. Hiyo ni kweli? Sisi ni warithi wa vitu vyote. Biblia ndiyo kwanza imekwisha kusema hilo hapa. Sisi ni warithi wa vitu vyote, kila kitu. Hatunayo bado, bali ni yetu. Amina. Loo, utukufu! Mimi sina hata inchi moja ya ardhi, bali yote ni yangu, kwa vyo vyote vile. Hakika. Yote ni yetu, mali ya watu, Kanisa, waaminio, Bibi-arusi wa Kristo anamiliki kila chembe yake. Urusi inaipigania, Marekani

inaipigania *hiyo*, na huyu akipigania *hii* na *hii* upande ule, na halafu wanatuita “wenda wazimu.” Tulienu tu, ni mali yenu, kwa vyo vyote vile. Amina. Yote tutairithi, hata hivyo, kwa hiyo acha wagombane na kulipuana. Ni yetu. Sisi ndio tunaoipata. Wao hata hawawezi kuwazia juu yake, bali tunaiwazia, haidhuru. Tunaiwazia, haidhuru!

<sup>68</sup> Ni nani angeliwazia ya kwamba maskini mzee yule pale, maskini hao ng’ombe wazee waliokonda, wenye mifupa mitupu kule juu ya kilima, alimiliki vitu vyote? Palestina yote ilikuwa ni yake. Naam, bwana. Kwa hiyo alipofikia mahali ambapo shindano la kuamua lilipokuja, Mungu alithibitisha kuwa pamoja naye. Alilichukua kundi hilo dogo la wanaume akatoka kwenda huko na kuwapiga kila mmoja wao, na akarejesha mali yake. Amina. Ninapenda hilo. Kwa nini? Aliweka imani yake juu ya Mwamba wa ahadi ya Mungu. Hilo ndilo linalohitajika. Yeye hakujenga msingi mwingine, kwenda kujiunga na dhehebu fulani wala kupata kitu kama hiki. Aliweka imani yake juu ya Ahadi hiyo! Amina. Ndiyo hiyo, kwenye hiyo Ahadi, na hapo akasonga mbele! Upanga ulioingia kutu ama usio na kutu, haukuleta tofauti yoyote kwake, alikuwa ameweka imani yake juu ya ile Ahadi.

<sup>69</sup> Na wewe unapokuja mbele kuombewa, kama unataka wokovu, kama unataka uponyaji wa Kiungu, haidhuru ni kitu gani, kama wewe ni mwaminio, wewe ni mrithi wa kila ahadi. Kwa hiyo weka imani yako juu ya ahadi na usonge mbele, na umwambie Shetani, “Rudisha! Rudisha! Ni yangu.” Usimwache akudanganye. Simama papo hapo mstarini, atairudisha. Mungu alisema atairudisha, kwa hiyo lazima kuirudisha. Hayo ni mamlaka yako. Hiyo ni kweli, mrithi wa vitu vyote!

<sup>70</sup> Yeye alidumu kwenye msingi huo, Neno lililoahidiwa, naye alikuwa na mrithi. Alikuwa ndiye mrithi, kwa hiyo alijua jambo hilo. Vema, bwana, baada ya hiyo ahadi kuthibitishwa kwake, yeye alifanya ushirika na Mwenye Kuahidi (ninapenda hilo) baada ya Mungu kufanya ahadi. Na halafu basi, unaona, Ibrahimu hakuwa amejaribiwa hapo awali, kwa hiyo yeye. . . la namna hiyo. Kwa hiyo alijua yote yalikuwa ni mali yake, na hiyo ilikuwa ndiyo ahadi, hata hivyo haikuwa imembidi kupigana na jeshi. Hakuja lolote kuhusu jambo hilo. Ha—hakuwa mtu aliyefundishwa kupigana. Ibrahimu hakuwa mpiganaji, alikuwa mkulima. Wala Ibrahimu hakuweza kufanya jambo lolote, kwa sababu yeye—yeye hakuwa askari. Watu wake hawakuwa askari, walikuwa wakulima. Kwa hiyo jambo pekee angaliweza kufanya lilikuwa ni kuchukua tu ahadi ya Mungu, kuweka imani yake juu ya ahadi na kutoka, kwenda kulifuatilia. Ndipo wakati Ibrahimu alipoona jambo hilo, na kupata ahadi hiyo, na kuona kwamba Mungu alimthibitishia jambo hilo, ya kwamba Yeye kweli hutimiza ahadi Yake. . . Amina! Hiyo hapo.

<sup>71</sup> Kama bado kabisa hujampokea Roho Mtakatifu, hujui kitu chochote juu Yake, na kitu fulani moyoni mwako kinakwambia ya kwamba unamtaka, kaa papo hapo. Huo ni Uzima wa Milele, huo ndio unaorithi. Kaa papo hapo, na umwangelie Shetani moja kwa moja usoni na kusema, “Wewe ndiwe mwizi, ni wewe! Nimekuja kumiliki yale Yesu aliyonifia niyapate, sasa yarudishe! Simile!”

<sup>72</sup> Ndipo, jambo la kwanza unajua, Roho Mtakatifu atamiminika juu yako. Ndipo jambo fulani linatukia. Jambo fulani litatukia. Ni kitu gani? Mungu alithibitisha hushikilia Neno Lake. Hiyo ni kweli kabisa. Halafu, angalia, ndipo baadaye unaona Neno limethibitishwa kwako, ya kwamba umeokoka, una Roho Mtakatifu, halafu kitu gani? Ibrahimu alikuwa amepata ushindi, huyu hapa anarudi akitembea kiaskari, alikuwa akishuka kwenda, huku imani yake imewekwa juu ya Neno ya kwamba angeweza kukirudisha, kile alichokuwa amepoteza, na huyu hapa anarudi nacho, akipiga hatua za mshindi. Hilo ndilo jambo lile lile unaloweza kufanya. Kama huna Uzima wa Milele, mwombe Mungu. Kiri dhambi zako, mwamini Mwana wa Mungu, kubali Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na useme, “Mungu, ninamjia, niko hapa kumpokea.” Ndipo urudi, mwendo wa mshindi. Unaye. Amina. Unaangaza tu, jamani, ndege wanaimba tofauti, na kila mtu... Ndipo unampenda kila mtu. Ile chuki ya zamani, kijicho, ugomvi vimeondoka. Wampenda kila mtu! Loo, unakuwa tu na wakati wa furaha sana, ukiimba, ukipaza sauti, ukimsifu Mungu. Hujali yale mtu yeyote anayosema kukuhusu wewe. Yote ni mema. Hakika, unatembea mwendo wa mshindi!

<sup>73</sup> Basi ni Nani aliyetoka kuja kumlaki? Ni Nani aliyetoka kuja kumlaki? Melkizedeki. Melkizedeki alitoka akaja kumlaki baada ya kulithibitisha Neno Lake. Melkizedeki Ndiye aliyempa Neno. Ndipo akaweka Neno lake... imani yake juu ya Neno, akapata ushindi kisha akarudi, ndipo akafanya ushirika. Amina. Sasa, utafanya hivyo, pia. Loo, Neno Lake litakuwa kitu kipya kwako, wakati wowote mara utakapopata ubatizo wa Roho Mtakatifu. Loo, jamani!

<sup>74</sup> Loo, unasema, “Siwezi kuona mambo haya. Siamini katika kupaza sauti. Siamini katika kunena kwa lugha. Siamini katika uponyaji wa Kiungu.” Inaonyesha wewe kabisa hujapata ushindi. Hiyo ni kweli. Lakini wakati mmoja utakapopata ushindi, ndipo umeupata. Basi unao. Ndiyo, bwana, ndipo unaweza kupaza sauti. Mimi... .

<sup>75</sup> Mmeona wakati mmoja nilikuwa nikifikiri juu ya kucheza katika Roho, kuona mtu fulani akisimama na kucheza katika Roho. Sasa, nimeona uigaji ukifanywa juu yake, bali nimeona kitu halisi, pia. Kwa hiyo, nilikuja kuona, kwa nini watu waliweza kucheza katika Roho? Vema, sijapata bado kuona mmoja akifanya yasiyofaa, sijaona mmoja bado akitenda

maovu. Daima ni—ninaliona likifanywa kwa heshima tu na kwa utaratibu na utamu, na hata wenye dhambi wanakimbilia madhabahuni na kuokoka wakati linapoendelea. Vema, nilishangaa ni kwa nini ilikuwa hivyo, ndipo nikaja kutambua ilikuwa ni ushindi.

<sup>76</sup> Daudi alicheza mbele za Bwana, wakati sanduku la agano liliporudishwa kwenye mahali Pake pa kupumzika. Amina. Wakati Daudi alipoliona Neno, kama lilivyokuwa kwenye vibao vya mawe wakati huo, limerudishwa mahali pake sahihi, Daudi alishangilia na kucheza katika Roho, akazunguka na kuzunguka na kuzunguka. Kwa nini? Aliona Neno limerudishwa mahali pake. Amina.

<sup>77</sup> Kile Neno linachohitaji, si kutoka kwenye seminari fulani, mchanganyiko fulani wa kitheolojia; bali ni mhubiri wa mtindo wa kale, aliyetumwa na Mungu akiwa nyuma ya mimbara, akiwa na Neno, tukiona Mungu akilithibitisha, kulihakikisha.

<sup>78</sup> Ndipo Daudi akasema, “Utukufu kwa Mungu, jambo ndilo Hili!” Akazunguka na kuzunguka na kuzunguka na kuzunguka. Maskini mke wake mwenye kiburi ameketi pale, akiwa ni binti ya mfalme, kasema, “Mbona, a—a—ananiaibisha.”

<sup>79</sup> Ndipo Daudi akasema, “Ati hupendi hilo? Angalia hili!” Basi akazunguka na kuzunguka tena. Naam! Loo, jamani, ni wakati wa jinsi gani aliokuwa nao!

<sup>80</sup> Unajua, Mungu aliangalia chini kutoka Mbinguni, akasema, “Daudi, wewe ni mtu unayeupendeza moyo Wangu.” Unaona? Unaona? Kwa nini? Alikwisha kupoteza majivuno yote, alikwisha kupoteza mambo yake yote. Hata hivyo alikuwa amemwoa binti wa mfalme, bali hilo hata halikufikiwa wakati huo. Alijua ya kwamba alikuwa anamjua Muumba wa Mbingu na nchi, na hapa lilikuwapo Neno la Mungu likirudi moja kwa moja miongoni mwao tena, naye Daudi alikuwa na furaha sana hata akacheza. Alicheza tu kwa nguvu alivyoweza.

<sup>81</sup> Miriamu, alinyakua tari akashuka akaenda ufukoni, akicheza kwenye ng'ambo ya pili. Baada ya kupita kwenye Bahari ya Shamu na kuona adui zake wamekufa maji, basi aliweza kucheza katika Roho. Wakati alipoona adui waliokuwa wamemtesa, wamekufa, ndipo akacheza katika Roho. Naam. Sasa, unaona, baada! Baada ya kushinda vita, ndipo utukufu wa Mungu hushuka.

<sup>82</sup> Sasa, tunaona ya kwamba alimlaki. Na baada ya ahadi kuthibitishwa, a—alikuwa na ushirika. Melkizedeki alitoka akaja kumbariki Ibrahimu, na Yeye akasema, “Abarikiwe Ibrahimu, na abarikiwe Mungu wa Ibrahimu, Muumba wa Mbingu na nchi.”

<sup>83</sup> Loo, jamani, jinsi ninavyopenda jambo hilo, ahadi ya mwaminio! Unasema, “Hilo lina uhusiano gani na sisi?” Kwa kila mwaminio! Ahadi ya mwaminio ni Uzima wa Milele.

Ahadi ya mwaminio ni Uzima, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, saburi, matunda ya Roho, uponyaji wa Kiungu, mambo dazani moja niliyoandika hapa chini, karibu hivyo, ambayo ni mali yako. Ni yako, bali huwezi kuwa nayo mpaka utakapoyapigania. Ni yako. Kila kitu kinachoonekana, kila kitu cha kawaida ambacho kinaonekana, ni changu. Mungu alinipa mimi, kwa sababu kwa kupitia Kristo Yeye alinipa mimi. Na vitu visivyoonekana ni vyangu. Amina. Ninapenda hilo! Yale unayoweza kuona, kama vile uponyaji wa Kiungu, kadhalika, namna hiyo, ambayo ni mema, hayo tunayafurahia; bali yasiyoonekana!

<sup>84</sup> Sasa, sayansi inaweza kuchunguza hapa na kusema, “Vema, hebu tuone, hebu nimchukue mtu huyu. Ulisema aliponywa, hebu nimchukue nimpeleke kule chini nikamchunguze. Hebu nione kilichotukia. Ati unasema ulikuwa na uvimbe wakati mmoja, bwana?”

“Naam, papo *hapo*.”

<sup>85</sup> “Vema, hebu nitoe utafiti wa kisayansi na tuone kama haukudidimia ndani tu wala haukuondoka. Unasema wakati mmoja ulikuwa kipofu na sasa unaona. Ninajuaje? Hebu niangalie kisayansi nione hilo.”

<sup>86</sup> Sasa, wangeweza kuchunguza kote juu ya hilo, lakini hata hivyo mi—mimi ni mrithi wa hilo, pia, kila kitu cha kimwili. Na halafu mimi ni mrithi wa vitu visivyoweza kuonekana pia, ambapo sayansi haiwezi kuchunguza. Amina. Amina. Vitu visivyoonekana, amina, mimi ni mrithi wake. Naam, bwana. Vitu vinavyoweza kuonekana, mimi ni mrithi wake. Dunia ii hii, mimi ni mrithi, wewe ni mrithi. Kila mwaminio ni mrithi, yeye ni mrithi wake. Vema, halafu yasiyoonekana! Ati Mwenye Kumiliki nini? Mbingu na nchi. Amina. Vitu vyote! Je! unaamini jambo hilo?

<sup>87</sup> Unasema, “Ndugu Branham, na je! huko nje ambako huwezi kuona? Unajuaje?” Kungali ni kwangu. Hiyo ni kweli. Mbingu ni yangu. Nafurahi ni yangu, Mungu alisema hivyo. Na hiyo ni kweli. “Vema, hujapata kuona, unajuaje iko?” Ninajua iko, kwa vyo vyote vile, Mungu alisema hivyo. “Unajuaje wewe ni mrithi wake, wakati hujapata kuona?” Ninaamini Neno Lake. Amina. Unaona? Mimi ni mrithi, wewe ni mrithi pamoja nami, sisi sote ni warithi pamoja kwa njia ya Kristo Yesu.

<sup>88</sup> Je! uliona hapa katika Wakorintho hapa, katika Wakorintho wa Pili, Paulo alisema, hata kuhusu mauti, tunamiliki mauti. Wazia jambo hilo. Ati kumiliki mauti? Naam, bwana, inatutii. Amina. Vema, utukufu! Tayari nimesahau kuhusu ule mlipuko wa bunduki sasa, unaona. Kwa nini yeye hakuniua? Kwa sababu asingeweza. Hiyo ndiyo sababu. Mungu hakuwa tayari. Angeweza kuja kadiri anavyotaka kuja, bali hawezi kukuchukua. Amina. Utukufu! Nililipa deni langu la jambo hilo

muda mrefu uliopita wakati nilipomwamini Yesu Kristo ambaye yu hai milele na milele. Sasa mauti husikiliza yale tunayosema. Amina.

Unasema, “Ati mwenye kumiliki mauti?”

<sup>89</sup> Hilo ndilo Paulo alilosema hapa katika Wakorintho. Mauti, hata hiyo, tunaimiliki. Mbona, wakati walipokuwa wakijiandaa kukata kichwa chake, yeye alisema, “Ee, mauti, u wapi mwiba wako? U wapi mwiba wako? Nionyeshe mahali unapoweza kunitisha.”

<sup>90</sup> Mauti ikasema, “Nitakukaba na kukuweka chini kaburini, nawe utaoza na kuharibika.”

<sup>91</sup> Yeye akasema, “Lakini, loo, Mungu ashukuriwe,” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Naam, bwana. Mauti, kuzimu, na kaburi, ninavimiliki vyote, kwa sababu Yeye alivishinda vyote kwa ajili yetu. Mwenye kumiliki!

<sup>92</sup> Ni kama tu vile Yoshua na Kalebu walivyorejea na ushahidi wa ile nchi isiyoonkana iliyokuwa wamepewa watu hao kwa ahadi. Yoshua na Kalebu walirudi na ushahidi ya kwamba kulikuwa na nchi kama hiyo. Sasa, hapa chini walikuwa na ahadi yake. Mungu aliwapa ile ahadi, nao wakaja moja kwa moja kwenye nchi hiyo, bali hawakuwa wamepata kuiona, nao Yoshua na Kalebu walienda kwenye nchi hiyo ya ahadi na kurudisha ushahidi ya kwamba hiyo nchi ilikuwa ipo na ilikuwa ni nchi nzuri, iliyojaa maziwa na asali. Amina! Ilikuwa ni kitu gani? Walikuwa wakienda kuimiliki nchi hiyo. Walikuwa na ahadi. Walikuwa njiani wakielekea kule, nao walikuwa karibu sana na Yordani, ndipo Yoshua akavuka na kuleta ushahidi ya kwamba ilikuwa ni nchi nzuri.

<sup>93</sup> Vile tu Yoshua alivyowafanyia wana wa Israeli, (*Yoshua* linamaanisha “Mwokozi,” neno Yoshua), na hilo ndilo jambo lile lile Yesu alilifanyia Kanisa wakati walipomwua. Alishinda mauti. Alishinda kuzimu. Alishinda kaburi. Na akafufuka tena akiwa na thibitisho, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ya kwamba kuna Nchi ng’ambo ya mto, wanayoiita ya furaha milele. Amina. Yeye alirudi na kutuletea ushahidi. Huo unafanya nini, Ndugu Branham? Unakufanya uache kusema uongo, kuiba, kunywa pombe, kulaani, maovu, kila kitu. Unakufanya kiumbe kipya. Mimi ambaye wakati mmoja nilikuwa nimekufa katika dhambi na makosa, hata hivyo mimi ni hai, si mimi bali ni Kristo anayeishi ndani yangu. Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu, amina, mrithi wa ahadi. Haleluya! Naam, bwana. Hiyo nchi ni yetu. Unajuaje? Yoshua alifufuka kutoka katika wafu, akarudi na thibitisho, Roho Matakatiifu. Ninaye. Amina. Whiu! Utukufu! Mimi ni mrithi. Loo, mtoto wa Mfalme, mtoto wa Mfalme, mrithi wa vitu vyote! Biblia ilisema hivyo. Mungu yeye yule—Mungu yeye yule aliyewapa Israeli ahadi ya nchi ya ahadi

(ilikuwa ni kitu kisichoonekana kwao), Biblia iyo hiyo, Mungu yuyo huyo alitupa ahadi ya Uzima wa Milele, na Roho Mtakatifu anashuhudia jambo hilo. Kristo yu hai, hajafa. Anaishi moja kwa moja miongoni mwetu, anaishi ndani yetu, kupitia sisi, anafanya kazi pande zote kutuzunguka. Amina.

<sup>94</sup> Ilikuwa ni Yeye aliyekuwa ameketi kwenye benchi lile kule hivi majuzi wakati Shetani alipoona nafasi ya kuniua, lakini asingeweza kufanya jambo hilo. Amina. Naye hatafanya hivyo kamwe mpaka Kristo atakaposema mambo yako tayari. Amina. Haidhuru atakuja mara ngapi, atarudi mikono mitupu mpaka Kristo atakapotoa amri. Amina. Ahadi, Mungu aliahidi jambo hilo. Ni Neno la Mungu ndilo linaloahidi hilo, nasi tunaliadini kwa sababu sisi ni warithi.

<sup>95</sup> Mimi ni mrithi wa uponyaji wa Kiungu. Mimi ni mrithi wa furaha, nina haki ya kufurahi. “Kwa hiyo ni kitu gani kinachokufanya uwe na furaha jinsi hii?” Nina haki ya kufurahi. “Unajuaje?” Kwa sababu mimi ni mrithi wake. Amina! Whiu! Sasa najisikia kuwa mtu wa dini. Naam. Mimi ni mrithi wa furaha. Mimi ni mrithi wa shangwe. Mimi ni mrithi wa amani. Mimi ni mrithi wa Uzima wa Milele. Mimi ni mrithi wa Roho Mtakatifu. Amina. Mimi ni mrithi wa kila ushahidi alio nao. Amina. Mimi ni mrithi wa mamlaka ya Mungu. Amina. “Ni nani aliyekufanya hivyo?” Sio mimi, Yeye alinifanya hivyo. Kila mmoja wenu ni mrithi wa kitu kile kile.

<sup>96</sup> Mrithi wa kiti cha enzi! “Yeye ashindaye ataketi pamoja Nami kwenye Kiti Changu cha Enzi, kama nilivyoshinda na kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Baba Yangu.” Amina, mrithi wa vitu vyote! Si kitu kimoja tu; vitu vyote! Kila kitu kiko chini ya miguu yako. Hata mauti iko chini ya miguu yako, kaburi liko chini ya miguu yako, kuzimu kuko chini ya miguu yako, dhambi iko chini ya miguu yako, kila kitu kiko chini ya miguu yako. Wewe ni mrithi! Nawe umeninii... Umekufa, na uhai wako umefichwa katika Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, nawe umefufuka tena kuingia katika Uzima wa Milele, na umeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Loo, jamani! Whiu! Tuite chochote unachotaka, tuite unachotaka, sema sisi ni wenda wazimu ukitaka, bali sisi ni warithi. Warithi wa nini? Vitu vyote.

<sup>97</sup> “Je! wewe ni mrithi wa Maskani ya Branham?” La, mimi ni mrithi wa vitu vyote. Vyote pamoja vinavyoonekana, vilivyopo, vijavyo, wa kila kitu, mimi ni mrithi wake.

<sup>98</sup> Na kila dhambi na uovu vimewekwa chini ya miguu yangu, kwa neema ya Yesu Kristo. Yeye alifufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, akashinda mauti, kuzimu na kaburi, na kunifanya mrithi, na kusema, “Ngojeni kule Nami nitawapa ile ahadi.” Na mtumishi Wake aliyetiwa mafuta na mwenye mamlaka alisema, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, kwa wote

walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Mimi ni mrithi. Amina. Amina. Yesu alithibitisha jambo hilo kwetu, katika kufufuka Kwake. Loo, jamani.

<sup>99</sup> Tukisha kuingia kwenye uwanja huo wa vita kati ya mauti na Uzima! “Mimi ni mwenye dhambi, Ndugu Branham.” Si lazima uwe. Wewe ni mwenye dhambi kwa sababu unataka kuwa. Si lazima uwe. Deni imekwishalipwa.

<sup>100</sup> “Ndugu Branham, laiti ningalikuwa na furaha.” Unaweza kuwa nayo. Unamwachilia tu Shetani akunyang’anye baraka ambazo Kristo alizifia. Mimi ni mrithi wake. Yote ni yangu. Kila kitu alichokifia, ni mali yangu, ni mali yako. Sisi ni watoto Wake, sisi ni warithi wake, kila kitu alichofia.

<sup>101</sup> Sasa, unapoingia kwenye uwanja huo wa vita. “Aha, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unajua, uta—uta—utafanya mambo ya upuzi. Na kutakuwako na kitu fulani, kutakuwako na kitu fulani tofauti.” Sijali ni tofauti vipi, mimi ni mrithi wake. Huo ni Uzima, nami ninakuja kuutwaa. Hiyo ni kweli.

<sup>102</sup> Hiyo ndiyo inayopaswa kuwa nia ya kila mwenye dhambi. “Ninakuja kuipokea juu ya msingi wa Roho Mtakatifu ambaye yupo hapa sasa na ananiambia nije na kumpokea. Ni wangu. Sitaamka mpaka nitakapompokea. Sitakuwa mshupavu wa dini. Nitakaa papa hapa, sijali ni kitu gani kinachotendeka. Sitaacha kuomba mpaka Wewe utakaponipa Roho Mtakatifu, Bwana, nami ninajua utafanya hivyo sasa hivi. Kukiweko na jambo lolote baya maishani mwangu, niambie habari zake nami nitalifanya. Liwe ni nini, Bwana, nitaliweka sawa.”

<sup>103</sup> Kama Mungu hafunui lolote, sema, “Basi, Shetani, ninakuja kumpokea. Huwezi kusimama pale tena, nipishe!”

<sup>104</sup> Haya basi, mrithi wa vitu vyote. Mrithi wa Uzima wa Milele. Mrithi wa uponyaji wa Kiungu. Loo!

Mrithi wa wokovu, chombo cha Mungu,  
Nimezaliwa kwa Roho Yake, nikaoshwa katika  
Damu Yake.

Hii ndiyo hadithi yangu, na huu ndio wimbo  
wangu,  
Kumsifu Mwokozi wangu siku nzima.

Utii mkamilifu, yote ni shwari,  
Mimi katika Mwokozi wangu nina furaha na  
kubarikiwa;  
Nikisubiri na kungoja, na kuangalia juu,  
Nimejazwa na wema na upendo Wake.

Haleluya! Haya basi. Hii ndiyo hadithi yangu, na huu ndio wimbo wangu. Mimi ni mrithi wa wokovu. Wokovu ni nini? Kitu ambacho umepewa. Ni zawadi. Mimi ni mrithi wa wokovu. Wa namna gani? Kwa Uzima wa Milele. Wokovu kwa ajili ya

nafsi yangu, wokovu kwa ajili ya mwili wangu, wokovu kwa ajili ya uchovu wangu, wokovu wa kila kitu. Mungu alinifanya mrithi wa kila kitu kupitia Kristo, na Yeye alikufa, akafufuka, kisha akarudi na kuleta ushahidi, na kummimina juu yetu. Loo, jamani! Utukufu! Loo, jamani!

<sup>105</sup> Sasa, unaenda kule juu, unafanya nini? Unapokwenda tu kama vile Ibrahimu alivyofanya, unakwenda kule ukiwa na ahadi hiyo. “Mungu, Wewe uliniambia ni yangu. Nina imani katika ahadi Yako. Ninaleta Neno Lako. Uliahidi jambo hili. Ulisema, ‘Ombeni, nanyi mtapewa. Tafuteni, nanyi mtapata. Ombeni, nanyi mtapewa. Bisheni, nanyi mtafunguliwa.’ Mimi hapa, Bwana. Nipo hapa. Ninabisha, ninatafuta, ninaomba. Sina budi kumpokea.” Haya basi. Jambo fulani linatukia basi, loo, wakati unapolitekeleza hilo Neno.

<sup>106</sup> Angalia kile Shetani alichofanya wakati Yesu alipoliweka Neno juu yake. “Na pia imeandikwa...” Aliruka mbali na Waya huo, kama nilivyosema hivi majuzi usiku. Naam, bwana. Ndipo nini, baada ya wewe kushinda? Unashindaje? Ungeweza kufanya jambo hilo peke yako? La. Mtu fulani alikutangulia na akakushindia. Ni Kristo. Mimi ni mrithi wake tu. Hainibidi kufanya lolote. Mimi ni mrithi wa hiyo ahadi. Kitu pekee ninachopaswa kuwa nacho, ni kuweka imani yangu juu ya ahadi Yake. Unalionwa?

<sup>107</sup> “Ndugu Branham, je! wewe unastahili jambo hilo?” La. “Je! unafikiri mimi ninastahili?” La. “Je! unafikiri Askofu anastahili?” La. “Je! kuna mtu wakati wowote anayestahili?” La. “Vema, kwa nini?” Wewe ni mrithi.

<sup>108</sup> Kama ulikuwa u mlevi mkubwa sana ulimwenguni, na baba yako alikuachia dola milioni moja, kama unastahili ama hustahili, m—m—mrithi wake, wewe ndiwe mrithi wa urithi wa Baba yako. Chochote alichokuachia, ni chako haidhuru kama unastahili ama hustahili. Alikuachia. Amina.

<sup>109</sup> Nilikuwa mwenye dhambi, lakini mimi ni mrithi. Nilikuwa sifai, bado, bali ningali ni mrithi. Ninapaswa kufa na kwenda kuzimu, bali mimi ni mrithi. Mimi ni mrithi wa nini? Uzima wa Milele. “Unajuaje utaupata?” Niliuhisi. Roho Mtakatifu aliuleta. Yesu alifufuka katika wafu kusudi upate kuja. Na sasa umekuja, na unashuhudia na kuthibitisha vile vile kabisa alivyosema ungefanya. Nimepita toka mautini kuingia Uzimani. Nimekuwa, kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Kwa hiyo mimi ni mrithi. Naam, bwana. Sasa niko safarini mwangu. Amina. Vitu vinauawa. Mambo hayo yote mabaya niliyofanya ni nini? Ni kama tu vile Miriamu alivyofanya. Aliangalia huko nyuma, hayo hapo, yamekufa, yamezikwa katika bahari ya usahaulifu, katika Kitabu cha Kitabu kikuu cha Mungu Mbinguni. Imekwisha. Jina langu tayari limewekwa kwenye Kitabu hicho, na tayari kimetiwa muhuri, na kuwekwa kwenye bahari ya usahaulifu, na

Kitabu kipya, kilicho na jina jipya lililoandikwa Utukufuni. Na ni langu. Naam. Sasa sisi ni warithi wa vitu vyote, basi.

<sup>110</sup> Ndipo kama vile ambapo Ibrahimu, je! Mungu alimwambia nini? “Nchi hii ni yako. Kilicho ndani ya hii ni chako. Angalia mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini, yote ni yako, kila kitu hapa. Ninataka uje usafiri katika nchi ya kigeni, nami nitakufanya mrithi wa nchi hiyo. Nitakupa hii, wewe na uzao wako, baada yako milele.” Sasa, Ibrahimu, jambo pekee alilopaswa kufanya lilikuwa ni kuweka imani yake kwenye ahadi hiyo, atwae upanga wake na aondoke. Hapo ule wakati muhimu sana ulipowadia, alishuka akaenda kule na Mungu akavipigana vita vyake. Na wakati alipopigana vita, aliwapiga hao wafalme.

<sup>111</sup> Naye huyu hapa alikuwa anarudi, amina, yote yamekwisha sasa. Ndugu, angeweza kupaza sauti. Wasikilize hao vijana wote wakipaza sauti na kumsifu Bwana! Huyu hapa Ibrahimu anakuja, na ni Nani anayejitokeza kuja kumlaki? Melkizedeki, Mfalme wa Salemu. Na hebu angalia waliyofanya. Baada ya vita kwisha, wangeweza kuketi chini na kula mkate na divai. Mfalme alitoa mkate na divai. Mbona alimfanyia hivyo? Baada ya vita kwisha, baada ya kupatikana kwa ushindi, ndipo waliweza kuketi chini na kula ushirika pamoja, kuzungumziana na kula ushirika pamoja. Loo, hilo ndilo Mungu analotaka watoto Wake wafanye usiku wa leo.

<sup>112</sup> “Basi vipi kukuhusu wewe, Ndugu Branham? Vipi kuhusu Kanisa hilo unalolihubiria?” Sisi ni uzao wa Ibrahimu, wao ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Sisi ni uzao wa Ibrahimu, kwa ahadi, kupitia kwa Kristo Yesu tunakuwa uzao wa Ibrahimu na sisi ni warithi pamoja naye kulingana na ahadi. Basi kama Ibrahimu alikuwa ni mrithi, mimi ni mrithi. Mimi ni mrithi pamoja na Ibrahimu, na wewe pia. Na ilitokeaje? Kupitia kwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ambao ulikuwa ni Kristo Yesu, Yule aliyeahidiwa, kwa imani. Ibrahimu alimpokea mwana, kama aliyetoka kwa wafu. Nasi tulimpokea Mwana ambaye hata hakuwa ni mwana, wala hana njia ya kufika hapa, na Mungu alimwumba na kumtuma kwetu. Naye akaja na kulipa adhabu ya dhambi zetu, na kwa mauti Yake ninakuwa mrithi. Loo, jamani. Haya basi. Na uovu wote wa ibilisi umeshindwa. Mungu asifiwe!

<sup>113</sup> Kushinda! Ni wangapi wameshinda, usiku wa leo? Hebu tuone mkono wako, “Kwa neema ya Mungu nimeshinda.” Mungu asifiwe. Mnajua kile ninachofikiri tunapaswa kufanya sasa hivi? Ninaanza tu kuzungumza moja kwa moja hapa na kuwaweka nusu ya usiku. Hebu na tufanye tu ibada nzuri ya kujiweka wakfu, tuyaweke wakfu upya maisha yetu kwa Mungu. Ni wangapi wanajisikia kufanya hivyo? Loo, nina zaidi ya mmoja sasa, nimeinua mikono yote miwili juu, na moyo wangu, pia. Ninataka maisha yangu yazungumze kwa niaba ya Kristo. Ninataka kujiweka wakfu upya kwa Kristo.

Ninataka mapenzi Yake yafanyike, yangu yawekwe nyuma, na—na mapenzi Yake yafanyike. Ninataka kuwa na mwendo wa mshindi. Si kwa sababu ni mimi; kwa sababu ninajua ya kwamba Injili aliyohubiri inaumia siku hizi kwa sababu ya mafundisho ya masharti ya kimadhehebu ya kujibunia na kadhalika. Ule ushindi mkuu tunaopaswa kuwa nao umezuiliwa na adui. Mungu, jalia niuvute upanga huu, jalia umetamete na ung'are, na nisonge mbele. Jalia mapenzi yangu yawe nyuma, na Neno Lake likitangulia namna hiyo, Upanga mkali ukatao kuwili ukifanya njia.

<sup>114</sup> Hebu tusimame kwa miguu yetu sasa na tujiweke wakfu upya. Kila mmoja kwa njia yako mwenyewe, jiweke wakfu kwa Bwana. Na tuinue mikono yetu sasa kwa Mungu, kila mmoja.

<sup>115</sup> Baba yetu wa Mbinguni, usiku wa leo tunajiweka wakfu Kwako vizuri kabisa tujuavyo. Tunajua ya kwamba sisi ni warithi wa vitu vyote. Uliahidi jambo hilo, Bwana Yesu, nasi tunaliadini. Sasa, kamwe hatutaweza kulifanya hilo isipokuwa Wewe, Bwana... isipokuwa sisi wenyewe tuweke imani yetu kwenye ahadi Yako. Sasa, Wewe ulisema, katika Biblia, “Aulaye Mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu anao Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali atapita... amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Aulaye Mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu anao Uzima wa Milele, Nami nitamfufua katika siku ya mwisho.” Hiyo ndiyo ahadi. Hivyo ndivyo Wewe ulivyosema. Hivyo ndivyo tunavyoamini.

<sup>116</sup> Na, Bwana Mungu, Ee Roho Mtakatifu, tenda kazi juu yetu. Loo, tenda kazi, Mungu! Tenda kazi, Ee Bwana, ndani yetu. Roho wa Mungu aliye hai, tupokee, Bwana. Katika Jina la Kristo tupokee. Nisafishe, nifinyange, niumbe, Ee Mungu, katika mfano wa Mwana wa Mungu. Nitwae, Bwana, Mimi ni Wako. Ninakupa kanisa hili. Ninatoa kila nafsi hapa Kwako, pamoja na yangu, Bwana. Sasa tuumbe na utufinyange, na jalia tusahau njia zetu za dhambi na mbaya, na tujue mradi tu tunaweka imani ye—yetu, imani tuliyo nayo, juu ya Neno Lako lililoahidiwa, utatuchukua kupita kutoka ushindi hadi ushindi. Umeahidi jambo hilo.

<sup>117</sup> Shetani hawezi kutudhuru, Bwana. Angeweza kufanya jambo lolote awezalo kufanya, wala hawezi kutugusa. Wakati ulipomwachilia juu ya Ayubu wakati mmoja, Wewe ulisema, “Usiutwae uhai wake.” Yeye alifanya kila kitu ila kuutwaa. Bali asingeweza kufanya jambo hilo, kwa kuwa ahadi Yako ilikuwa ingali pale kwa Ayubu.

<sup>118</sup> Na, Mungu, Wewe ungali ni Mungu yeye yule leo. Unawalinda walio Wako. Tunajua ni Kweli, nasi tunajiweka wakfu upya. Osha nafsi zetu zenye dhambi, Bwana, tunapokiri imani yetu. Na, Kristo Yesu, tupokee. Na wakati tunapoanza kushiriki meza hii ya Bwana, Mungu, nena nasi mioyoni mwetu. Tuambie sasa mahali tumekosea. Tuonyeshe mahali kosa letu

lilipo, Bwana. Tunalitubu kwa unyenyekevu. Kwa unyenyekevu ninaweka dhambi zangu zote juu ya madhabahu, Bwana. Kwa unyenyekevu ninajilaza mwenyewe juu ya Neno Lako, Bwana, na kwenye rehema Yako.

<sup>119</sup> Nipo hapa, Bwana, fanya nami utakavyo. Hicho ndicho kilio cha kanisa hili, Bwana, “Fanya nasi utakavyo.” Ninaweza tu kuzungumza juu ya—juu ya nafsi yangu, Bwana, bali ninaamini mioyoni mwao wanaamini jambo lile lile. Fanya nasi utakavyo. Tunaamini. Tunataka kuwa warithi, nasi tunajua ya kwamba sisi ni warithi mradi tu tunakaa katika Kristo Yesu. Sisi ni warithi pamoja Naye mbele ya Kiti cha Enzi.

<sup>120</sup> Sasa kuwa pamoja nasi. Yaponye magonjwa miongoni mwetu, Bwana. Kama kukiwapo na mwili ulio mgonjwa hapa usiku wa leo, uguse, uponye, upe afya. Tujalie, Bwana. Kukiwako na nafsi inayougua, na iponywe sasa hivi. Jalia nafsi hiyo iliyoulemaa inyoshwe. Jalia magoti hayo manyonge yanayoning’inia chini na hiyo mikono dhaifu iinuliwe katika utukufu na makelele kwa Mungu. Jalia njia zilizopindika zinyoshwe. Na kuwe na njia kuu nyikani kwa ajili ya Mungu wetu.

<sup>121</sup> Bwana, tunaamini Wewe unakuja hivi karibuni, na jalia tulitangaze Neno Lako, Bwana, na tufanye njia kuu nyikani, mahali palipopindika panyoshwe, kwa ajili ya Bwana wetu. Na tulipulie mbali kila shina la kimadhehebu. Na tulipulie mbali kila shina la uchungu, tulipulie mbali kila namna ya uovu, husuda na ugomvi, kusudi Neno la kweli la Mungu litiririke kama mito ya furaha. Tujalie, Baba. Tunajitoa Kwako sasa kabla tu hatujashiriki Meza hii ya Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>122</sup> Wakati, Dada Spencer anataka maombi kwa ajili ya mwili wake! [Dada Spencer anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mungu akubariki, Dada Spencer.

Baba wa Mbinguni, maskini mwanamke huyu mtakatifu, na huyu ambaye ameketi. Unamwona mwanamke kiwete. “Na huyu binti wa Ibrahimu haikumpasa afunguliwe siku ya Sabato?” Na sasa huenda wengi wa marafiki wake, Bwana, marafiki wa kale ambao alikuwa akiwakaribisha, hao wahudumu, walipoketi ndani ya nyumba yake, wamwekwisha kuaga dunia, wengi wao, wamekwisha kupitia kwenye barabara kuu ya kwenda Mbinguni. Ameachwa peke yake, Bwana, kama ushuhuda. Hakuna mtu sasa, ni watoto wake tu, na labda rafiki fulani hapa na pale, Bwana, jamaa fulani mara kwa mara. Lakini anasimama peke yake kama msitu mkubwa ambao umepeperushwa ukaanguka chini, na mti mmoja ukabaki. Mungu, ninaomba ya kwamba utaangalia chini kwa rehema, Bwana, ya kwamba ameimarika sana. Na amesimama juu ya mlima wa Kalvari, Bwana, akiwa na shina na msingi katika

Imani ya Kristo. Ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu mkongwe mpendwa na kulaani kifundo hiki chini ya ulimi wake, ya kwamba kimwache na afanywe mzima. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Mungu akubariki. Asante, Dada Spencer. Itafanyika. Usitilie shaka tu hata kidogo. Vema.

Imani yangu inakutumainia Wewe,  
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,  
Mwokozi wa kiungu;  
Sasa nisikie ninapoomba,  
Ziondoe dhambi zangu zote,  
Wala usiniache nipotee  
Kutoka Kwako kwenda kando.

Sikilizeni, imbeni pamoja nami sasa.

Wakati nikipitia mashaka ya giza ya maisha,  
Na huzuni imenizunguka,  
Wewe uwe Kiongozi wangu;  
Amuru giza ligeuke kuwa mchana,  
Pangusa huzuni na machozi,  
Loo, hebu nifanye Wako kabisa,  
Tangu leo!

<sup>123</sup> Kutoka kwenye kilindi cha moyo wako sasa, Mungu tu ndiye anayejua hilo, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, kweli unamaanisha ya kwamba, “Jalia tangu leo, Bwana, niwe Wako kabisa”? Hebu na tuimbe hiyo sehemu ya mwisho tena.

Wala usiniache nipotee  
Kutoka Kwako kwenda kando.

<sup>124</sup> Sasa sote pamoja. Mchungaji Mkuu wa kundi, Wewe ulitufundisha ya kwamba tunapaswa kuomba namna hii. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaomba pamoja—Mh.] Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe. Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani, kama huko Mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Na utusamehe dhambi zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu; kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina. Mwaweza kuketi.

<sup>125</sup> Nimeombwa maombi kwa ajili ya mtoto wa Dada Shepherd. Ndiyo kwanza nikumbuke ya kwamba walipiga simu muda kidogo uliopita kwa ajili ya maombi ya mtoto huyo, nami nikamwombea. Nilikuwa nifanye mazungumzo ya faragha papa hapa, wala nisingeweza kupitia nyumbani. Bali walisema maskini msichana huyo mdogo alikuwa mgonjwa na alikuwa na homa, na kwa namna fulani kukakamaa, ambako hapana shaka ni kirusi tu kinachozunguka. Mnajua kuhusu hilo. Wakati mwingine misuli yao inajivuta ndani hivi kwamba inakubidi kuikunjuakunjua kwa mikono yao, kama vile Bibi Haley na wengi hapa chini. Ni kirusi kinachozunguka. Naye... niliomba dua. Nami nilisema kama mtoto huyo mchanga hakupata nafuu

zaidi ifikapo saa tatu ama kwenye wakati tutakapofunga ibada, wapige simu hapa nasi tungewapitia, kama mtoto huyo mchanga alipata nafuu, sawa. Kwa hiyo hebu kwa unyenyekevu tu sasa, kabla hatujakula ushirika, tumwombe mtoto huyo.

<sup>126</sup> Bwana Yesu, mtoto huyo mchanga, sijui ana umri gani wala chochote kile, bali ni mmoja wa wanafunzi wetu wapendwa hapa, Bwana, mmoja wa waaminio wetu. Ni mtoto wao, wa Dada Shepherd na Ndugu Shepherd, lulu ndogo ambayo umewapa, Bwana. Tunaomba ya kwamba utamwangalia, na kumbariki na kumlinda, na kumponya na kumpa afya. Tulin dai sasa hivi. Baada ya Ujumbe huu, tunam dai huyo. Tunam dai kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kulingana na Neno Lake. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia ugonjwa umwachilie mtoto huyo. Na jalia mtoto huyo apone na awe mzima, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa limenenwa, sasa litatendwa. Amina. Mnaamini?

Kama tukiamini wala kamwe tusitilie shaka,  
hakika atakufanikisha;

Mpelekee Bwana mizigo yako na uiache pale,

Iache pale, loo, iache pale,

Mpelekee Bwana mizigo yako na uiache pale;

Ukiamini wala usitilie shaka, hakika  
atakufanikisha;

Mpelekee Bwana mizigo yako na uiache pale.

(Hivyo ndivyo tu unavyofanya.)

Kama mwili wako unaumwa sana na huwezi  
kupata nafuu tena,

Kumbuka tu Mungu Mbinguni hujibu maombi;

Sasa, Yesu anajua uchungu unaohisi, Yeye  
anaweza kuokoa na anaweza kuponya;

Mpelekee Bwana mzigo wako na uuache.

<sup>127</sup> Sasa hebu na tupeane mikono sisi kwa sisi tunapoimba ubeti huu wa mwisho.

Uuache pale, (ushirika, unajua, ushirika)  
uache pale, (Bwana asifiwe!)

Mpelekee Bwana mzigo wako na uuache pale;

Iwapo tutaamini wala tusitilie shaka, hakika  
atakufanikisha;

Mpelekee Bwana mzigo wako na uuache pale.

<sup>128</sup> Loo, si Yeye ni wa ajabu? Sasa, sasa pamoja na kukiri kwetu, imani yetu, kukiri dhambi zetu, tukiamini ya kwamba dhambi zetu zote zimo katika bahari ya usahaulifu. Yeye atakayekiri dhambi zake, Mungu ni mwenye haki kuzisamehe. Unaona? Zimo kwenye—kwenye bahari ya Damu ya Yesu Kristo, wala kabisa hazitakumbukwa tena. Ni wangapi wenu enyi wanawake mnaojua dawa ya kuondoa madoa ni nini? Ninyi nyote. Sasa, hebu na tuchukue beseni kubwa iliyojaa Kloroksi; hiyo ni dawa moja ya kuondoa madoa, beseni kubwa mno

iliyojaa Kloroksi. Halafu utachukua kidude cha kudondoshea matone, nawe una tone moja la wino mweusi kwenye kidude hicho kidogo, hizo ni dhambi zako. Simama moja kwa moja juu ya beseni hilo, ukiminye kuelekea chini, ndipo uangalie chini kwenye beseni hilo uuone. Imekuwaje? Wino umekuwaje? Wakati ulipogusa hiyo dawa, ilikuwa na nguvu sana iliondoa tu hiyo rangi kutoka kwake, hauwezi kuwako tena. Ni kitu gani? Imetoweka, imepotea milele. Ni kitu gani? U—ule wino wenyewe umekuwa Kloroksi. Hiyo ni Damu ya Yesu Kristo kwa kila dhambi iliyotubiwa. Ni kitu gani? Imesahauliwa, imemalizika, imekwisha, imesamehewa, imetalikiwa, imeondolewa mbali. Haiwezi kabisa kukumbukwa dhidi yako tena.

<sup>129</sup> [Dada mmoja anazungumza kutoka kwenye kusanyiko—Mh.] Mtu fulani anaita jina langu, mahali fulani. [Dada huyo anashuhudia kuponywa kwake wakati uo huo.] Vema, Bwana asifiwe! Angali hai! Bwana ashukuriwe. Tunamshukuru Bwana. Ee Mungu, jinsi tunavyokusifu kwa wema Wako. Naam, maskini mtu mnyenyekevu huko nyuma alingusa, Bwana alingusa. Vema. Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.

<sup>130</sup> Kumbukeni, kila neno ni Nanga, imara na ya hakika. Hakuna ninii. . . Unaona? Weka tu imani yako moja kwa moja juu yake wala usisogee, kaa tu pale. Sasa, huwezi kuiweka pale chini halafu uinyakue tena na kusema, “Nitaijaribu tena.” Iweke pale. Kaa moja kwa moja pale pamoja nayo. Naam, bwana. Kama vile Habili alivyofanya, ufe kabisa kwa mawazo yako mwenyewe. Sema tu, “Mungu, ni Neno Lako, si vile ninavyowazia. Ni Neno Lako. Hilo hapo.” Naye Habili alikufa kwenye Mwamba. Na, kwamba, Yeye atagusa tu kama vile alivyomgusa dada pale. Ni rahisi tu kabisa.

<sup>131</sup> Tunajaribu kuifanya. . . Hatuninii. Shetani hujaribu kuifanya kuwa ngumu sana, unajua, kusema, “Loo, unajua, hilo lilikuwa ni kwa ajili ya siku iliyopita,” na yote hayo. Hao ni wasioamini tu.

<sup>132</sup> Bali kwenu ninyi mnaoamini, Yeye ni wa thamani. Sasa amekataliwa, kweli; bali Yeye ni Jiwe la thamani likilijia Jiwe lililo hai, Jiwe la thamani, Jiwe Kuu la Pembeni. Loo, jamani. Loo, yeye aligusaye jiwe hili huponywa! Hivyo tu. Amina.

<sup>133</sup> Sasa, hivi hatuna shukrani kwa Bwana? Tuna furaha tu, nina furaha sana ya kwamba Bwana ni Mungu. Amina. Nina furaha sana ya kwamba Yeye ni Baba mpole, mwingi wa rehema, hulireshimu Neno Lake, akitimiza Agano Lake, bila kulisahau. Yeye hutimiza Agano Lake. Hana budi kulitimiza, Yeye ni Mungu, Yeye alilifanya. Yeye ni Chemchemi ya Kweli yote. Unaona? Haiwezekani kuwe na jambo lingine lolote ila Ukweli usioghoshiwa wakati wote. Kila Neno analosema haliwezi kukosea. Na hili ni Neno Lake. Na, Ee Mungu, jalia imani yangu

iwe isiyoweza kukosea ndani Yake, amina, ndipo inaweza kuwa isiyokosea kama vile Neno lisivyoweza kukosea, ndipo Neno katika imani ya namna hiyo litazaa chochote ambacho Neno linasema litazaa. Amina. Kwa hiyo, nisafishe, Bwana. Nijaribu, nisafishe, niponye, nilinde, nibariki, na unipe rehema Zako, ndiyo maombi yangu kwa Mungu. Amina.

<sup>134</sup> Sasa, nitasoma sehemu ya Neno sasa, linalopatikana katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, kifungu cha 23.

*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi pia, ya kuwa Bwana Yesu usiku . . . aliotolewa alitwaa mkate,*

*Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Chukueni, na mle; huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*

*Na vivi hivi yeye akatwaa . . . akakitwaa kikombe, na baada ya kula, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; hii iwe ndani yenu, fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*

*Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata atakapokuja.*

*Basi kila aulaye mkate huu, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya damu, mwili na damu ya Bwana.*

*Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.*

*Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.*

*Kwa sababu hiyo wako wengi kweni walio hawawezi na dhaifu, . . . watu kadha wa kadha wamelala.*

*Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.*

*Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.*

*Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, ngojeni mmoja na mwingine, ngojaneni;*

<sup>135</sup> Sasa hebu niseme jambo hili. Yesu alitupa amri hii kabla hajaenda kwenye mauti Yake, akijua ya kwamba alikuwa akienda kule. Wanafunzi wangali wakishangaa kile alichokuwa akizungumzia, walipoandika hili. Lakini Yeye alisema, “Kikombe hiki ni Agano Jipya la Damu Yangu. Fanyeni hivi kila mwulapo na kukinywea, mnaonyesha mauti Yangu hata nitakapokuja.” Loo, hayo Maneno ya thamani!

<sup>136</sup> Hao wanafunzi hapana shaka walishangaa, “Yeye anamaanisha nini, ‘kuonyesha mauti Yake’? Tunawezaje kufanya jambo hili?” Hili hapa lilikuwa ni fumbo kabisa kwao, bali sio Kwake. Yeye alikuwa ni Mungu. Alijua yale yaliyompasa kufanya. “Kuonyesha...” Kwa hiyo alisema, “Mkutanikapo kula...”

<sup>137</sup> Sasa, “Yeye alaye na kunywea, isivyostahili,” anakuja hapa na kukiri kuwa Mkristo, akila Mwili wa Bwana, kisha anatoka anaenda na kuishi pamoja na ulimwengu na—na kumkana Kristo na nguvu Zake, na mambo kama hayo, u—unamfedhehi Mungu kabisa. U—unamfedhehi Kristo, kwa hiyo usiule. Bali kama unajaribu kwa yote yaliyo ndani yako, kuishi vyema na kuonyesha ya kwamba wewe ni Mkristo, ya kwamba unampenda Yesu Kristo, basi ni jukumu lako kufanya hivyo.

<sup>138</sup> Na sasa katika... Ninaamini ni Yohana Mtakatifu, mlango wa 6, Yesu alisema, “Yeye aulaye Mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa milele, Nami nitamfufua katika siku ya mwisho.” Sasa, ahadi hiyo, hilo si ni jambo zuri sana? “Nitamfufua.”

<sup>139</sup> Je! ulipata kuwazia wewe upo hapa kwa sababu gani? Kwa nini ninyi—kwa nini ninyi mnaenda shuleni, watoto? Kwa nini unafanya kazi, baba? Ni kitu gani kinachokufanya uamke, na mama, asubuhi, na kuwapeleka watoto shuleni, unaosha uso wao, na kutengeneza vitanda na kupika, na—na—na kufanya hayo yote? Unaingia, umechoka sana usiku huo, na kesho yake unaanza jambo lile lile. Unafanya hivyo kwa sababu gani? Kwa nini unashughulika na kufanya kazi ngumu, baba, na kila kitu? Unakuja usiku, na umechoka, na mmoja wa watoto anakuwa mgonjwa nawe unatembea hapa na pale sakafuni, na kulia na kuomba na kusumbuka, halafu wanapona; na kisha unarudi, na kufanya jambo hilo tena. Na kila Jumapili unaosha nyuso zao, na unawapeleka kanisani. Na, vema, hayo yote ni ya nini? Yeye yuko hapa kwa kusudi gani? Je! mambo ni hayo tu? Jamani, hiyo ingekuwa ni taabu tupu, na ukijua huna budi kwenda kwa vyo vyote vile. Unaona? Hayo yote yana maana gani?

<sup>140</sup> Loo! ndugu, ni wakati wa kuhoji, ni wakati wa kuitumia fursa! Ni nafasi ya kukubali Hili. Niambie jambo fulani litakalochukua mahali Pake. Niambie kitu kilicho bora kuliko Hilo. Toa chochote ulimwenguni, mtu kuwa mfalme wa dunia, kutawala ulimwengu, kuwa Krushev ama Kennedy, ama chochote unachotaka kuwa, hata hivyo utakufa. Sawa! Hujui hilo litakuja wakati gani, dakika yoyote. Lakini hapa, wakati mauti inapopiga, unao Uzima wa Milele wala huwezi kufa, ukiwa na hakikisho kwa Mungu wa viumbe vyote, Ambaye ni Muumba wa Mbingu na nchi, “Nitamfufua tena katika siku ya mwisho.”

<sup>141</sup> Nisaidie kutokuamini kwangu, Ee Mungu. Ijaze nafsi yangu, Ee Mungu, nisafishe, nijaze, niagize, nitume. Jalia nisife, jalia niishi nipate kusimulia Hadithi hiyo. Nijalie niende kwenye kila ufa na pembe ya nchi, na kulihubiri Neno na kupanda mbegu, naam, bwana, kusudi kuwe na mavuno katika siku ya mwisho, ya Neno la kweli lisiloghoshiwa, pamoja na waaminio katika Kristo.

<sup>142</sup> Je! dhambi zako ziko chini ya Damu, kwa imani usiku wa leo katika Kristo Yesu? Sasa tutakula ushirika. Si ushirika; mnashiriki mnapokula pamoja. Shiriki tu pamoja na Mungu. Ushirika sio huo mkate, sio divai, *ushirika* ni “kuzungumza pamoja na Mungu.” Na huu ni mfano tunaokula, ya kwamba tunaamini katika mauti Yake, mwili uliovunjwawunjwa, kuzikwa Kwake na kufufuka, tunaamini katika Uwepo wa Roho Mtakatifu. Nasi tunaamini ya kamba ametupa Uzima wa Milele wala hatuwezi kufa, tumepita kutoka mautini tukaingia Uzimani. Na siku moja tutakapotengana mmoja kwa mwingine hapa, tutafufuka tena katika ufufuo sisi kwa sisi, tukiunganishwa pamoja na Kristo Yesu, kama Mwili. Amina. Juu ya misingi hii, na kukiri dhambi zangu, na imani yangu katika Mwana wa Mungu, ninajichukua mwenyewe pamoja na kanisa mbele ya maagizo haya ambayo Mungu alituachia tufanye, kuonyesha mauti Yake hata atakapokuja.

<sup>143</sup> Yesu alisema, “Huu ni mwili Wangu uliovunjwawunjwa kwa ajili yenu. Kuleni, fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu.”

<sup>144</sup> Baba yetu wa Mbinguni, baada ya sisi kutubu dhambi zetu, kulisikia Neno Lako, baada ya kukiri ya kwamba sisi hatustahili, nasi tunatumaini tu katika ustahilifu wa Mwana wa Mungu. Sisi ni viumbe wasiostahili. Tusamehe, Bwana, kuhusu yote tuliyoifanya. Na sasa, kwa imani, tunakuja kwenye meza ya Bwana. Na sasa kwa kuwa mkate huu umetolewa kuwakilisha mwili wa Bwana wetu, ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utaitakasa kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa kwake. Na jalia kila mtu anayeushiriki huu awe na Uzima wa Milele katika nafsi yao. Na jalia ya kwamba kila mtu anayeula apate uponyaji mwilini mwao, na aishi wakati uliokusudiwa ambao umewapa. Na jalia wakutumikie siku zote za maisha yao, na wafufuliwe katika siku ya mwisho katika ufufuo, wapate kukusanyika pamoja na makabila ya dunia ambayo yamekombolewa kwa Damu ya Kristo. Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

<sup>145</sup> Biblia ilisema, “Pia alitwaa kikombe, na baada ya kula, akisema, ‘Hiki ni kikombe cha Agano Jipya, kila mnywapo hiki mnaonyesha mauti ya Bwana hata atakapokuja.’”

<sup>146</sup> Baba wa Mbinguni, tunashikilia Kwako tunda la mzabibu usiku wa leo, divai hii. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utaitakasa divai hii, inawakilisha Damu iliyomwagika

kwa ajili yetu pale Kalvari. Kupitia Damu hii tuna ondoleo la dhambi zetu, kwa imani katika kazi iliyomalizika ya Yesu Kristo. Tusamehe ninii zetu . . . kutokuamini kwetu kote, Bwana, na utupe imani na ufahamu, na utufanye watumishi Wako, Bwana, ili tuweze kukutumikia Wewe siku zetu zote. Kuwa pamoja nasi, Baba, tunapoungana pamoja kuizunguka meza hii, na utubariki katika ushirika huu mzuri na Meza ya Bwana pamoja na Wewe. Naomba uzungumze na mioyo yetu na utuelekeze kwenye kazi yetu tunayopaswa kufanya. Tujalie, Bwana. Takasa divai hii kwa matumizi iliyokusudiwa. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.



*KUMILIKI VITU VYOTE* SWA62-0506

(Possessing All Things)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza ulitolewa Jumapili jioni, tarehe 6 Mei, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)